Bismillahir Rahmaanir Rahiim

NUKUU ZA SOMO

KWA

UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

Elimu ya Dini ya Kiislamu

SHULE ZA SEKONDARI

KIDATO CHA PILI

Imeandaliwa

na

Islamic Education Panel

2013

Bismillahir Rahmaanir Rahiim

YALIYOMO Uk.

Neno la Awali ……4
Utangulizi ……..... 6

MADA YA 1.0
NJIA ZA KUMJUA MWENYEZI MUNGU …….. 7
Njia za Kumtambua Mwenyezi Mungu …… 7
Nguzo za Imani ……. 8
Zoezi la 1. ……. 11

MADA YA 2.0
MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA DINI ……... 13
Mtazamo wa Kikafiri juu ya Dini. ……13
Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini. …….. 14
Kwa nini Mwanaadamu hawezi kuishi bila dini. ……..16
Zoezi la 2. ……..17

MADA YA 3.0
MAMBO YA LAZIMA KUFANYIWA MAITI WA KIISLAMU. ……... 18
Kumkosha (Kumuosha) maiti. ……..20
Kumkafini (Kumvika sanda) maiti. ……..22
Kumswalia maiti. ……..25
Kumzika maiti. ……..28
Zoezi la 3. ……. 30

MADA YA 4.0
NGUZO ZA UISLAMU. ……....32
Shahada mbili. ……...32
Kusimamisha swala za Sunnah. ……...32
Zakat. ……35

Kufunga mwezi wa Ramadhani. …….....41
Funga za Sunnah. ……..43
Funga za Kafara. ……...44
Hijjah. ……46
Zoezi la 4. ……..55

MADA YA 5.0
QUR'AN. ……..57
Kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an. ……..57
Kusoma, kuhifadhi na kutoa mafunzo ya sura zilizochaguliwa. ……..58
Zoezi la 5. ……..62

MADA YA 6.0
SUNNAH NA HADITH. ……63
Uandishi wa Hadith za Mtume (s.a.w) katika vipindi vinne. ……63
Uchambuzi na Uanndishi wa Hadith Sahihi. ……68
Zoezi la 6. ……..71

MADA YA 7.0
BARA ARAB ZAMA ZA JAHILIYYAH KARNE YA 6 A.D. …….....72
Jiografia ya Bara Arab Zama za Jahiliyyah. ……71
Kuandaliwa Mtume (s.a.w). ……..74
Mtume (s.a.w) Kulingania Uislamu Makkah. ……...79
Zoezi la 7. ……..89

NENO LA AWALI

Shukurani zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu (s.w) Mola na Mlezi wa Walimwengu wote, Rehema na Amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na Swahaba zake na wale wote waliofanya, wanaofanya na watakaofanya jitihada za dhati katika kuusimamisha na kuuendeleza Uislamu katika jamii.

Tunatoa Shukrani za dhati kwa Allah (s.w) kutujaalia kuandaa na kutoa kitabu hiki cha NUKUU ZA SOMO ya Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa Walimu na Wanafunzi wa Kidato cha Pili kwa Wanataaluma walioko na wasioko mashuleni.

Lengo Kuu la Somo

Somo limekusudiwa kuwapatia Elimu na Ujuzi sahihi juu ya Uislamu wasomi na kuwaandaa kuwa waumini wa kweli watakaoweza kukiendea kila kipengele cha maisha yao ya kibinfsi, kifamilia na kijamii kwa kufuata vilivyo mwongozo wa Qur'an na Sunnah.

Lengo la NUKUU ZA SOMO

Lengo kuu la kuandaa na kutoa kitabu hiki cha NUKUU ZA SOMO ni kuwarahisishia Waalimu na Wanafunzi Kidato cha Pili kufundisha na kujifunza vizuri somo hili na kuweza kujiandaa vyema katika kuandaa na kufanya mitihani yao ya kati nay a mwisho.
NUKUU ZA SOMO zitatumika kama mwongozo baada ya Mwalimu na Mwanafunzi kusoma kwa kina kitabu cha kiada cha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, Kitabu cha Pili kwa ajili kuandaa vitini vya kufundishia au kujiandaa kwa ajili ya mitihani.

Muundo wa NUKUU ZA SOMO.

Kitabu hiki kimejumuisha mada zilizokusudiwa kumuwezesha mwanafunzi na msomaji mwingine kupata maarifa na ujuzi uliokusudiwa. Mada zilizoandaliwa humo zimetokana na fani kuu tano katika Kitabu cha 2 cha kiada cha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari ambazo ni;

1. Tawhiid
2. Fiqh
3. Qur’an
4. Sunnah na Hadith
5. Tarekh

Mada zote kuu na ndogo zimeandaliwa kwa kuzingatia na kufuata vyema MUHTASARI WA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU SHULE ZA SEKONDARI KIDATO CHA I - IV, 2012. Hivyo wanafunzi wa Kidato cha Pili na Wanataaluma wengine wanatarajiwa kunufaika na mwongozo huu.

Kila Mada kuu imetolewa Zoezi la kufanya kama njia mojawapo ya kufanya tathmini ya uelewa wa wasomaji juu ya yale waliyosoma na utekelezaji wake.

Ujuzi wa Somo la E.D.K. Kidato Cha Pili

Baada ya kumaliza Kidato cha Pili, mwanafunzi anatarajiwa kuwa na ujuzi wa;

1. Kupambanua njia za kumtambua Mwenyezi Mungu.
2. Kutambua haja ya dini kwa mwanaadamu.
3. Kufafanua mambo ya faradh kufanyiwa maiti ya kiislamu.
4. Kutambua swala za Sunnah.
5. Kufafanua utekelezaji wa nguzo ya Zakat, Swaumu na Hijja.
6. Kusoma, kuhifadhi na kueleza mafunzo ya sura zilizochaguliwa.
7. Kubainisha historia ya uandishi wa Hadith na sayansi ya Hadith za Mtume (s.a.w).
8. Kufafanua historia ya kuhifadhiwa Qur’an wakati wa Mtume (s.a.w).
9. Kufafanua mafunzo yatokanayo na historia ya Uislamu kipindi cha Mtume akiwa Makkah.

UTANGULIZI.

Elimu ndio fani aliyofaradhishwa nayo mwanaadamu mara tu baada ya kuumbwa ili aweze kuishi na kufikia lengo la kuumbwa kwake hapa Ulimwenguni, hanabudi kuwa na fani zote katika Elimu ya Mazingira na ya Muongozo, kukosa mojawapo hupelekea upungufu katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi yatakayopelekea kufikia lengo.

Hivyo Uislamu hautapata matunda yake mpake Elimu zote mbili ya Mazingira na Muongozo zisomwe na kutekelezwa sambamba kikamilifu.

Malengo Mahsusi ya Somo la E.D.K. Kidato Cha Pili

Baada ya kumaliza Kidato cha Pili, mwanafunzi aweze;

1. Kuelewa njia za kumjua Mwenyezi Mungu.
2. Kufahamu haja ya dini kwa mwanaadamu.
3. Kutekeleza mambo ya faradh kufanyiwa maiti ya kiislamu.
4. Kubainisha swala za Sunnah.
5. Kufahamu utekelezaji wa nguzo za Zakat, Swaumu na Hijja.
6. Kusoma, kuhifadhi na kueleza mafunzo ya sura zilizochaguliwa.
7. Kuelewa historia ya uandishi wa Hadith na sayansi ya Hadith za Mtume (s.a.w).
8. Kuelewa historia ya kuhifadhiwa Qur’an wakati wa Mtume (s.a.w).
9. Kujadili mafunzo yatokanayo na historia ya Uislamu kipindi cha Mtume akiwa Makkah.

Wabillah Tawfiiq

==========

MADA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

****

1.0 NJIA ZA KUMJUA MWENYEZI MUNGU (S.W).

- **Njia za Kumtambua Mwenyezi Mungu (s.w).**

  a) Nafasi ya Fitrah (maumbile).

  - Kila Mwanaadamu amepandikizwa hisia za kimaumbile zinazomtambua Mungu kupitia ujuzi wa kutambua mema na maovu.

  - Mwanaadamu akipatwa na raha au misukosuko na huzuni hukiri uwepo wa Mwenyezi Mungu (s.w).
    Rejea Qur'an (17:67), (30:30) na (91:7-8).

  b) Vipaji vya Binaadamu.

  - Vipaji vya akili na milango ya fahamu na fani zingine za elimu ni nyenzo pekee zikitumiwa vilivyo humuwezesha mtu kumjua Mola wake.
    Rejea Qur'an (3:190-191), (35:28).

  c) Nafsi ya mwanaadamu.

  - Mfumo mzima wa mwili wa mwanaadamu na utendaji wake wa kazi wa ajabu wa viunge mbali mbali vya mwili kama kuyeyusha chakula tumboni, msukumo wa damu mwilini, n.k. ni ishara tosha juu ya uwepo wa Mwenyezi Mungu (s.w).
    Rejea Qur'an (51:20-21)

  d) Mazingira.

  - Utegemezi na uhusiano wa kimahitaji ya kutumia rasilimali ya kuishi kati ya mimea, wanyama na binaadamu (ecological balance).

- Maumbile mengine kama mbingu, ardhi na yote yanayoonekana na yasiyooneka katika mazingira yanayotunguka.
  Rejea Qur'an (3:190).

e) Wahyi (Ufunuo).

- Wahyi ndio nyenzo kuu ya kumwezesha mwanaadamu kumtambua Mwenyezi Mungu (s.w) kwa usahihi unaotakikana.

- Elimu, vipaji na ujuzi au sayansi pekee haviwezi kumwezesha mwanaadamu kumtambua Mungu kwa baadhi ya maeneo, mfano nguzo za imani, n.k.

- **Nguzo za Imani.**

1. Kumuamini Mwenyezi Mungu.
2. Kuamini Malaika wake.
3. Kuamini Vitabu Vyake.
4. Kuamini Mitume Wake.
5. Kuamini siku ya Mwisho.
6. Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu.

1. Kumuamini Mwenyezi Mungu (s.w).

- Imani juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu ni jambo la kwanza kabisa kwa kila mwenye akili timamu kupitia ishara na maumbile mbali mbali yanayotuzunguka.
  Rejea Qur'an (3:190).

- Baada ya kumtambua, ni kumuabudu ipasavyo na kutomshirikisha katika sifa na majina yake matukufu na kiumbe yeyote.
  Rejea Qur'an (18:109), (31:27), (57:1-7), (59:22-24).
  Rejea Kitabu cha 2, EDK, Shule za Sekondari; Uk.8-16.

2. Kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu.

- Malaika ni viumbe wa Mwenyezi Mungu walioumbwa kutokana na nuru kwa lengo la kumtumikia Mwenyezi Mungu (s.w).

- Ni viumbe wa kiroho, wasio na jinsia, wenye mabawa na wenye uwezo wa kujimithilisha na kitu (kiumbe) chochote.

- Hawana matashi ya kibinaadamu kama kula, kulala, kunywa, kuchoka, kuugua na hawana hiari kwa kila wanachoamrishwa na Mwenyezi Mungu (s.w).
  Rejea Qur'an (16:49-50), (7:206) na (21:26-27).

3. Kuamini Vitabu vya Mwenyezi Mungu (s.w).

- Kuamini vitabu vya Allah (s.w) ni lazima kwa kila muumini wa kweli kama vilivyoainishwa katika Qur'an, ambavyo baadhi ni;
  a) Suhufi – aliyoteremshiwa Nabii Ibrahim (a.s) na Nabii Musa (a.s).
  b) Taurat – aliyoteremshiwa Nabii Musa (a.s)
  c) Zaburi – aliyoteremshiwa Nabii Daud (a.s)
  d) Injili – aliyoteremshiwa Nabii Isa (a.s) na
  e) Qur'an – aliyoteremshiwa Nabii au Mtume Muhammad (s.a.w).

- Vitabu hivi vimeteremshwa kwa lengo la kuwaongoza wanaadamu katika njia sahihi na iliyonyooka ya maisha yao ili kufikia lengo la kuumbwa kwao.
  Rejea Qur'an (57:25) na (5:46).

  - ***Sababu ya Vitabu Vilivyotangulia kutajwa ndani ya Qur'an:***
    - Qur'an ndiyo Kitabu cha mwisho kilichoteremshwa kwa ajili ya kuwaongoza walimwengu wote.
    - Vimetajwa ili kuwafahamisha waislamu juu ya uwiano, usahihi na upotofu wa mafundisho hayo na yale ya Qur'an.

- Mwenyezi Mungu (s.w) kutaka kuonyesha nafasi na utata wa vitabu hivyo kutumika zama hizi kama mwongozo wa maisha.
- Mwenyezi Mungu (s.w) kutaka kuonyesha upungufu, mabadilisho na upotofu uliofanywa ndani ya Vitabu hivyo.
  Rejea Qur'an (6:92), (2:75), (4:14), (5:15), (5:48) na (16:64).

4. Kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu (s.w).

- Mitume ni wanaadamu wanaume walioteliwa ili kuwaongoza na kuwa mifano bora ya kuigwa kwa watu (ummah) wao katika kutekeleza ujumbe wao.

- Idadi kamili ya mitume wote wa Mwenyezi Mungu (s.w) haijulikani, bali waliotajwa ndani ya Qur'an ni 25.
  Rejea Qur'an (10:47), (6:83-86)
  Rejea Kitabu cha 2, EDK, Shule za Sekondari; Uk.23.

- **Sifa za Mitume.**
  i. Ni watu walizaliwa, walioa, walikula, waliugua, walikufa, n.k. kama binaadamu wa kawaida isipokuwa Nabii Adamu (a.s).
  ii. Walikuwa na kila tabia njema, wakweli, waaminifu na wenye huruma.
  iii. Walikuwa na upeo wa Elimu wa hali ya juu kuliko watu wote enzi zao kwa sababu kuletewa kwao wahayi.
  iv. Walikuwa Wacha-Mungu wa hali ya juu kuliko watu wote.

- **Kazi za Mitume.**
  i. Kufahamisha na kufundisha juu ya uwepo wa Mwenyezi Mungu (s.w) na sifa zake. Qur'an (21:25), (16:36).
  ii. Kufahamisha mambo ya ghaibu (Akhera) kama Moto, Pepo, Kiyama, Hisabu, Maisha ya Barzaq (kaburini) n.k.
  iii. Kufundisha njia sahihi ya maisha anayoiridhia Mwenyezi Mungu inayopelekea kunusurika na adhabu zake. Qur'an (3:164).

iv. Kusaidiana na wafuasi wao katika kuamrisha mema na kuondosha maovu katika jamii.

v. Kuonya kutokana na adhabu na kubashiria mema kwa wafanyao mema.

5. Kuamini Siku ya Mwisho.

- Ni kuwa na yakini moyoni kuwa kuna maisha mengine baada ya kufa.
  - ***Hatua za maisha baada ya kufa:***
    a) Kutokwa na roho.
    b) Maisha ya kaburini (Barzaq).
    c) Kufufuliwa.
    d) Kuhesabiwa (Hisabu).
    e) Kuishi Peponi au Motoni milele
       - Kwa mujibu wa amali zao (vitendo vyao).

6. Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu (s.w).

- Ni kuwa na yakini moyoni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w) anao mpango wa viumbe vyake vyote alioweka kabla ya kuumba chochote.

- Amekiumba kila kiumbe kwa lengo maalumu na kukikadiria mahitaji yake yote. Rejea Qur'an (11:6), (57:22), (54:49) na (25:2).

Zoezi la 1.

1. (a) Bainisha njia kuu tano zinazomuwezesha mwanaadamu kumtambua Muumba wake.
   (b) Taja nguzo za Imani kwa mtiririko wake.

2. (a) Orodhesha Vitabu vilivyotajwa ndani ya Qur'an pamoja na Mitume walioteremshiwa kwayo.
   (b) Eleza, kwa nini Vitabu hivyo vimetajwa ndani ya Qur'an?

3. Ainisha sifa za Mitume wa Mwenyezi Mungu (s.w) kama ulivyojifunza katika somo hili.

4. Nafasi ya mwanaadamu imetofautiana sana na viumbe wengine, bainisha ni vitu au sifa gani zinazomtofautisha mwanaadamu na viumbe wengine.

5. Onyesha majukumu makuu ya kuletwa Mitume wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa Ulimwenguni.

6. Maisha baada ya kufa ni jambo lisilobudi kwa kila mwanaadamu, taja kwa mpangilio hatua za maisha ya mwanaadamu katika kuelekea maisha ya Akhera.

2.0 MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA DINI

- **Mtazamo wa Makafiri juu ya Dini.**

Mtazamo wa kikafiri juu ya dini uko katika sehemu kuu tatu zifuatazo;

a) Maana ya dini.
b) Chimbuko, Asili au Chanzo cha dini.
c) Kazi ya dini katika jamii.

1. Maana ya dini.

- Ni imani juu ya kuwepo Mungu Muumba Muweza na Mwenye nguvu juu ya kitu. Rejea tafsiri ya neno '*Religion*' katika Kamusi ya Kiingereza.

"Belief in the existence of a supernatural ruling power the creator ....."

Tafsiri:

"Dini ni imani ya kuwepo Mungu Muumba aliyemuweza na mwenye nguvu....."

2. Chimbuko, Chanzo au Asili ya dini.

- Makafiri wanadai kuwa chimbuko la dini linatokana na mawazo na fikra finyu za mwanaadamu alipokuwa katika maisha ya ujima (primitive age).

- Dini ni fikra na dhana alizoibua mwanaadamu baada ya kushindwa kutatua matatizo ya kijamii, uchumi, siasa, n.k.

- Dini ni dhana iliyoibuliwa na mwanaadamu kutokana na uduni wa maendeleo ya sayansi na teknolojia.
  Rejea kitabu cha Kafiri, *F. Angels* kiitwacho *'Anti-Duhring'*

"*Religion arose from primitive conceptions of men……*"

Tafsiri:

"Dini imeibuka kutokana na ujima (uduni) wa mawazo ya mwanaadamu……"

(c) Kazi ya dini katika jamii.

Ukirejea historia ya Ulaya na nchi za Magharibi, Kanisa kama dini lilitumika kwa kazi zifuatazo;

- Ni chombo kinacholeta unyonyaji, ukandamizaji na dhuluma katika jamii.
  Rejea Qur'an (28:4).

- Ni chombo cha kuleta matabaka na ubaguzi kati ya viongozi (mabwana) na waongozwa, matajiri na masikini katika jamii.

- Pia dini inaaminika kuwa ni chombo cha kulinda na kutetea maslahi ya watawala kupitia mafundisho yake.

- Dini inatumika kama chombo cha kuchuma na kujilimbikizia mali kwa wakuu (viongozi) wake kwa kuwatumia wafuasi wake.

- **Udhaifu wa Mtazamo wa Makafiri juu ya Dini dhidi ya Mtazamo wa Uislamu.**

Katika Uislamu dini maana yake ni mfumo, utaratibu, mila kamili wa maisha unaofuatwa na wanaadamu.
Rejea Qur'an (3:83), (3:85), (18:20), (9:33) na (16:9).

Tofauti na Makafiri, Uislamu unatazama dini kama ifuatavyo:

a) Maana ya Dini.
b) Chimbuko, Chanzo au Asili ya Dini.
c) Kazi ya Dini katika jamii.

(a) Maana ya Dini.

- Dini ni mfumo, utaratibu kamili wa maisha unaofuatwa na wanaadamu. Kinyume na mtazamo wa makafiri kuwa dini ni imani juu ya kuwepo Mungu Muumba.

- Hivyo, dini ni utaratibu wowote ule wa maisha wanaofuata watu (mtu) katika kuendesha maisha yake, sio lazima kuamini kuwepo wa Mungu Muumba.
  Rejea Qur'an (109:1-6), (9:31), (25:43), (61:8-9) na (17:81).

(b) Chimbuko, Asili au Chanzo cha Dini.

- Dai la makafiri kuwa chimbuko la dini limetokana na fikra finyu na uduni wa maendeleo ya sayansi na teknolojia wakati wa ujima, sio sahihi kwa sababu;

  - Hakuna kipindi chochote cha maisha, mwanaadamu aliishi katika ujima na fikra finyu, kwani tangu mwanaadamu wa mwanzo alipewa elimu na fani juu ya kuyamudu mazingira yake.

  - Pia mwanaadamu kila zama aliletewa mwongozo sahihi wa maisha kupitia mafundisho ya mitume unaotoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w).
    Rejea Qur'an (2:31) na (2:38-39).

- Hivyo katika Uislamu, chanzo na asili ya dini ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kwa ushahidi wa aya na hadith mbali mbali.

(c) Kazi ya Dini katika jamii.

- Mtazamo wa Makafiri, dini ni chombo cha unyonyaji, dhuluma na kujenga matabaka katika jamii, dai hili ni la kweli au sio la kweli kama ifuatavyo;

  - Ukweli wa dai hili ni sahihi kwa dini zote za wanaadamu kama Ushirikina, Utawa na Ukafiri.

- Udhaifu wa dai hili, ni kuwa dini sahihi ilikuwa na kazi ya kuikomboa jamii kutokana na aina zote za ukandamizaji, utabaka, dhuluma, n.k.

- Hivyo katika Uislamu, dini ina kazi ya kuiongoza jamii katika maisha ya haki, uadilifu na usawa na kupigana na aina zote za dhuluma na ukandamizaji.
  Rejea Qur'an (57:25), (28:4) na (7:103-105).

- **Kwa nini mwanaadamu hawezi kuishi bila ya dini?**

Mwanaadamu yeyote hawezi kuishi bila ya dini hata kama atadai kuwa hana dini kwa sababu zifuatazo;

1. ***Maana halisi ya dini.***
   Dini ni utaratibu wa maisha anaofuata mwanaadamu katika kuendesha maisha yake ya kila siku kibinafsi na kijamii.

2. ***Umbile la mwanaadamu ni la kidini.***
   Umbile la mwanaadamu limefungamana na kanuni na sheria za maumbile yote yanayomzunguka.
   Rejea Qur'an (30:30), (3:83).

3. ***Vipawa alivyotunukiwa mwanaadamu.***

   Tofauti na wanyama na viumbe wengine, mwanaadamu ametunukiwa vipawa vya ziada vifuatavyo;

   i. *Akili na Ufahamu wa hali ya juu.*
      Vinamsaidia kufikiri na kutafakari mambo yanayomhusu yeye mwenyewe na mazingira yanayomzunguka.

   ii. *Utambuzi binafsi (self-consciousness).*
      Humuwezesha kuhusianisha yeye na mazingira (viumbe) yanayomzunguka.

iii. Uwezo wa kujielimisha na kuelimika.

Elimu ni nyenzo pekee inayomuwezesha mwanaadamu kuyamudu mazingira kwa ufanisi.

iv. Uhuru wa kufanya atakalo.

Mwanaadamu amepewa vipaji, elimu na ujuzi, ilivimuwezeshe kubainisha njia sahihi ya kufuata katika maisha yake ya kila siku.

Zoezi la 2.

1. Eleza maana ya neno 'Dini' kwa mtazamo wa;
    (a) Kikafiri.
    (b) Kiislamu.
2. Eleza udhaifu wa mtazamo wa Kikafiri dhidi ya ule wa Uislamu juu ya;
    (a) maana ya dini.
    (b) asili au chanzo cha dini.
    (c) kazi za dini katika jamii.
3. Kwa mtazamo wa Uislamu, Dini ndio nyenzo pekee inayoweza kumkomboa mwanaadamu kwa kila aina ya utumwa. Eleza jinsi Dini ya Uislamu inavyoweza kumkomboa mwanaadamu na sio vinginevyo.
4. Bainisha sababu zinazomfanya mwanaadamu pamoja na ujuzi alionao hawezi kuishi bila ya dini (kufuata utaratibu wa maisha).
5. Taja vipawa alivyotunukiwa mwanaadamu na Mola wake vinavyomtofautisha na wanyama.

3.0 MAMBO YA FARADH KWA MAITI YA MUISLAMU.

3.1 Kuna aina Kuu mbili za Faradh.

- ***Fardh A'in.***

  Ni faradh inayomlazimu kila mtu binafsi kuitekeleza, haina uwakilishi.

  Mfano; kusimamisha swala, kufunga saumu, kuhiji, kutoa zaka, n.k.

- ***Faradh Kifaya.***

  Ni faradh ya kuwakilishana, wachache wakitekeleza hutosheleza hitajio.

  Mfano; kuswalia maiti, n.k. lakini akikosekana wa kuwakilisha, waislamu wote wanaohusika watawajibika.

3.2 Mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu.

- Kila nafsi itaonja mauti (kifo). Qur'an (3:185) na (4:78).

  Mambo manne yafuatayo ni lazima kufanyiwa maiti ya kiislamu:

  1. **Kuoshwa (Kukoshwa).**
  2. **Kuvikwa sanda (kukafiniwa).**
  3. **Kuswaliwa.**
  4. **Kuzikwa**.

Mambo muhimu anayofanyiwa Muislamu (mtu) anayekaribia kufa.

Mtu akikaribia kufa huwa hajiwezi kwa lolote lile pamoja na elimu, ujuzi alionao, hivyo huhitajia kufanyiwa mambo yafuatayo;

i. Kuogeshwa, kugishwa mswaki na kumpaka mafuta au manukato kama kuna uwezekano.
ii. Kumlaza kwa ubavu wa kulia au chali na kumuelekeza Qibla iwapo kuna uwezekano.
iii. Kumpa maji ya kunywa.
iv. Kutamka (kumsomea) – Shahada ***"Laa ilaha illallaah"***

   Abu Said na Abu Hurarirah wamesimulia kuwa, Mtume wa Allah amesema: *"Wasomeeni watu wenu wanaokaribia kufa;* ***'Laailahaillallaah"***

Pia Mu'az bin Jabal amesema kuwa Mtume (s.a.w) amesema: *"Yule ambaye maneno yake ya mwisho yatakuwa;* ***"Laailahaillallaah"*** *ataingia peponi.*

(Abu Daud)

- Si lazima anayekufa aitamke kwa sauti, inaweza ikawa kimoyo moyo.

Mambo anayofanyiwa mtu (maiti) mara tu baada ya kufa.

Baada ya mtu kufa inatuwajibikia tuseme: "Innalillah wainnailaihraaji'una". Qur'an (2:156). Kisha kumfanyia maiti mambo yafuatayo:

i. Kwa taratibu kurudishia mdomo wake usiwe wazi kwa kufunga kwa kitambaa kutoka kidevuni na kuzungushia kichwani.

ii. Kufunga macho ya marehemu na huku ukisema;

"*Kwa jina la Allah na kwa kufuata mila ya Mjumbe wa Allah, Ewe Mola wetu mrahisishie mambo yake ya sasa na msahilishie mambo yake ya baadaye. Na jaalia anayokutanayo yawe bora kuliko aliyoyaacha."*

iii. Lainisha viungo vyake (miguu na mikono) kwa kukunja na kukunjua taratibu.

- Kama kuna ugumu maji ya uvuguvugu au mafuta yanaweza kutumika kulaisha na kunyoosha viungo hivyo.
- Baada ya kulainisha viungo, miguu na mikono inyooshwe na kulazwa uso ukielekezwa Qibla kwenye mkeka au kitanda kisicho na godoro.

iv. Maiti avuliwe nguo zote alizokufa nazo na kisha kufunikwa kwa shuka kubwa

- Ni vyema afunwe kitambaa tumboni au kuwekewa kitu kizito ili tumbo lisifutuke.

v. Marashi na ubani vitumike kwa wingi ili kuzima harufu ya uvundo wa maiti.

- **Baada ya kufanyiwa hatua hizo, sasa ni lazima maiti kufanyiwa yafuatayo:**
  - Mambo haya ni faradh Kifaya, wakifanya wachache wanawakilisha wengine.

1. Kuoshwa (Kukoshwa).

- **Mazingatio kabla ya kuosha maiti.**

(a) Maiti ya kiume ioshwe na wanaume na maiti ya kike ioshwe na wanawake pia.
  - Maiti ya mtoto yaweza kuoshwa na yeyote.
  - Ni Sunnah mke kumuosha mumewe na mume kumuosha mkewe pia

(b) Ni mtu mmoja tu ndiye anayeosha na mwingine ni kwa ajili ya kumpa msaada inapobidi.

(c) Ni muhimu muoshaji afahamu masharti ya kuosha maiti muislamu kama vile;
  - Muoshaji awe muislamu.
  - Mahali pakuoshea pawe faragha (pamesitirika).
  - Maiti aoshwe huku amefunikwa gubi-gubi na nguo nyepesi inayoruhusu maji kupenya kwa urahisi.
  - Ni vyema muoshaji asiishike maiti bali aoshe akiwa amevaa ‘gloves’.
  - Kuzingatia masharti ya mwenye kuoga josho la wajibu; kama vile kuwa na maji mengi na safi, pasiwe na kizuizi cha maji kupenya, n.k.

(d) Ni muhimu muoshaji afahamu nguzo na sunnah za kuosha maiti kama ifuatavyo;
  - Nguzo za kuosha maiti ni mbili:
    - Nia
    - Kueneza maji mwili mzima wa maiti.
  - Ni Sunnah kumuosha maiti mara tatu au zaidi kwa idadi ya witiri.

- **Namna ya Kuosha Maiti hatua kwa hatua.**

  i. Maiti awekwe juu ya kitanda chenye tobo katikati ili kupitisha uchafu unaotoka tumboni.

ii. Pawepo na shimo (ufuo) usawa wa tobo la kitanda, kama hakuna uwekano chombo kiwepo cha kukingia uchafu unaotoka kwa maiti.
   - Pia maiti inaweza kuoshewa bafuni au kwenye karo liliotengenezwa kwa kazi hiyo.

iii. Maiti afunikwe na nguo moja kubwa yenye kupenyeza maji wakati wa kuosha.

iv. Maiti akalishwe juu ya kitanda usawa wa tobo na shimo (ufuo) na ainamishwe nyuma kidogo, kama ni mzito ni vizuri msaidizi wa muoshaji amuegemeze kwenye magoti yake.

v. Muoshaji apitishe mkono wa kushoto kwenye tumbo la maiti na kuliminyaminya taratibu ili kutoa uchafu ndani.

vi. Amlaze chali na kuminyaminya tumbo lake kama ilivyo mara ya kwanza.

vii. Aikalishe tena na apitishe mkono wa kushoto chini akiwa amevaa kitambaa au gloves na kusafisha tupu mbili kwa maji safi.
   - Kama hapaja takata, basi na avae gloves safi na ile chafu aitupe kwenye ufuo na asafishe tena kama mara ya kwanza mpaka patakate.

viii. Baada ya hapo, muoshaji afunge kitambaa safi kwenye kidole chake shahada na akichovye kwenye maji na kumswakisha maiti meno yote na kisha akitupe ufuoni.

ix. Muoshaji azungushe kitambaa kingine safi kidole chake kidogo mkono wa kushoto na kumsafisha nacho maiti tundu za pua kisha akitupe ufuoni.

x. Asafishe kucha za maiti kwa kijiti safi na laini iwapo ni ndefu na chafu.

xi. Kisha amkalishe maiti na amtawadhishe kwa kufuata taratibu za kawaida za kutia udhu (kutawadha).

xii. Maiti akiwa amekalishwa, ataanza kumuoshwa kichwa akiwa ameinamishwa mbele kidogo.
- Kama nywele au ndevu ni nyingi zichanwe na kuoshwa kwa sabuni na maji mpaka zitakate.
- Mwanamke mwenye nywele nyingi zisukwe mikia, na zilizong'oka ziambatanishwe na sanda.

xiii. Baada ya kuoshwa kichwa, maiti italazwa kwa ubavu wa kushoto na kuanza kuoshwa ubavu wa kulia, mbele na nyuma kwa pamoja kwa sabuni na maji safi mpaka itakate.

xiv. Kisha itaoshwa ubavu wa kushoto kama ilivyooshwa wa kulia.

xv. Baada ya makosho (maosho) haya mawili, la maji na sabuni na la kuondoa sabuni, kosho la tatu la maji liwekewe karafuu na marashi ili kulegeza viungo (maungo) vya maiti.

xvi. Baada ya makosho matatu haya, muoshaji anyooshe viungo vya maiti na kumlaza kama alikuwa mara tu baada ya kufa.

xvii. Kisha achukue nguo kavu na kumfuta maiti, na baada ya hapo maiti awekwe juu ya mkeka mkavu na kufunikwa kwa nguo kavu tayari kuvalishwa sanda (kukafiniwa).

2. Kumkafini (Kumvisha Sanda) Maiti.

- **Mazingatio juu ya Sanda.**
  - Ni sunnah kutumia nguo nyeupe.

‘Ibn Abbas amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema:

“Vaeni nguo nyeupe, kwa sababu hili ni vazi lenu lililo bora kuliko yote, na wakafinini maiti wenu kwa nguo (nyeupe)”

(Abu Daud, Tirmidh na Ibn Majah)

- Pia sanda isiwe nguo ya gharama.

  ‘Ali (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema:

  “Msigharamie sana nguo za sanda, kwani inakwenda kuozeana (kaburini)”

  (Abu Daud)

- Hajji akifa akiwa katika vazi la Ihram (Hija), vazi hilo ndio litakuwa sanda yake.

  ‘Abdullah bin Abbas amesimulia kuwa mtu mmoja alikuwa pamoja na Mtume (s.a.w) ngamia wake alimkanyaga, wakati akiwa anahiji mpaka akafa, Mtume wa Allah akasema:

  “Muosheni na maji na majani ya mkunazi na mumkafini kwa hayo mashuka yake mawili, msimpake manukato na msimfunike kichwa chake …….”

  (Bukhari na Muslim)

- Ukubwa wa sanda unategemeana na ukubwa wa maiti.

- **Sanda ya Mwanamume na namna ya kumkafini (kumvika).**
  - Sanda ya mwanamume ina vipande (majavi) vitatu.

    - ***Utaratibu wa kutayarisha sanda ya mwanamume.***

      i. Weka kipande cha kwanza juu ya mkeka kisha cha pili na cha tatu na vyote kushikizwa kwa uzi katikati, na kila kipande kipakwe marashi na ubani.

      ii. Pasua kamba katika pembe mbili za jamvi la kwanza, moja kwa ajili ya kufungia kichwani na nyingine kwa ajili ya kufungia miguuni.

Kamba moja itachanwa kutoka jamvi la pili, ili kumfunika (kufungia) maiti katikati. Na kamba tatu zitachanwa jamvi la tatu na la pili kwa ajili ya kufungia juu ya mkeka.

iii. Maiti italazwa juu ya majavi yote matatu. Ichukuliwe pamba iwekwe manukato kisha iwekwe juu ya viungo vyote vya sijda; paji la uso, viganja vya mikono, magotini na vidole vya miguu. Pamba itumike pia kuziba tundu zote mwilini; mdomo, masikio, pua na makalio.

iv. Maiti itatizwe (ifunikwe) mwili wote, kwa kuanza kipande cha kwanza, kisha cha pili na cha tatu ukitanguliza kunjo la kushoto kisha la kulia linafuata. Zile kamba zilizochanwa zitatumika kufungia vitanzi maiti kichwani, tumboni na miguuni. Baada ya hapo maiti inaweza kuwekwa kwenye jeneza baada ya kuzungushiwa kwa mkeka tayari kwa kuswaliwa.

- **Sanda ya mwanamke na namna ya kumvika.**

- Sanda ya mwanamke ina vipande vitano;
  - Majamvi 2
  - Shuka (Gagulo) au Underskirt 1
  - Kanzu (Blause) 1
  - Shungi (Ukaya) 1.

- ***Taratibu za kutayarisha sanda na kukafini:***

i. Majamvi mawili yatatandikwa moja baada ya nyingine.

ii. Kikatwe kitambaa cha ukubwa wa shuka ya kujifunga kiunoni (shuka/gagulo) na iwekwe juu ya majamvi mawili ili ije kutumika kumfungia kiunoni.

iii. Kisha ikatwe kanzu (blause) isiyoshonwa vizuri kwa kukunja kitambaa na kukitoboa katikati kwa ajili ya kuingizia kichwa cha maiti (kumvalisha) na kisha kushikiza pembeni kwa uzi mfano wa kanzu kata mikono na kuwekwa juu

ya gagulo sehemu ya chini (kiunoni) na itakuwa juu ya majamvi 2 sehemu ya juu (kifuani).

iv. Kitambaa (ukaya/shungi) ya kutosha kuweza kufunika kichwa na uso kitaingizwa ndani ya shingo ya kanzu na kunyooshwa kwa juu.

v. Maiti itaanza kuvalishwa kanzu, kisha kufungwa shuka (gagulo) juu yake. Kisha maiti itawekewa pamba viungo vyote vya sijda na kuziba sehemu za matundu kama ilivyokuwa kuwa kwa maiti mwanamume. Kisha maiti itatizwa (itafungwa) na majamvi mawili, moja baada ya jingine kwa kuanza kunjo la kushoto na kumalizia la kulia juu yake, na kisha kufungwa na kamba tatu juu yake- kichwani, tumboni na miguuni na kuwa tayari kuingizwa kwenye jeneza na kuswaliwa.

- **Sanda ya mtoto.**
  - Sanda ya mtoto mdogo, wa kike au kiume wasiofikia baleghe ni majamvi matatu, kama ilivyo sanda ya mwanamume.

3. Kumswalia Maiti.

- **Masharti ya Swala ya Maiti.**
  - Kwa wenye kumswalia maiti, watekeleze masharti ya kawaida ya swala.
  - ***Masharti ya maiti anayeswaliwa:***
    - Maiti awe muislamu
    - Maiti iwe imeoshwa na kukafiniwa
    - Maiti iwekwe mbele ya wanaoisalia.
      - Inajuzu kusalia maiti iliyo masafa ya mbali (swala ya ghaibu).

- Maiti zikiwa nyingi zipangwe mbele, za kiume zikiwa karibu na imamu kisha kusaliwa zote kwa pamoja.

o Maiti isiwe ya shihidi.

- Kwa mujibu ya Hadith ya Mtume (s.a.w), mashahidi hawaoshwi wala kusaliwa.

- **Nguzo za Swala ya maiti.**

- Swala ya maiti inaswaliwa wima; haina rukuu, sijda wala kikao.
- ***Nguzo za swala ya maiti ni;***

i. Nia
ii. Takbira ya kuhirimia
iii. Kusoma Suratul-Faatiha.
iv. Takbira ya Pili.
v. Kumswalia Mtume (s.a.w) kama tufanyavyo kwenye Tahiyyatu.
vi. Takbira ya Tatu.
vii. Kumuombea dua maiti.
viii. Takbira ya Nne.
ix. Kuombea dua waislamu wote, kisha kutoa Salaam.

- **Namna ya kutekeleza swala ya Maiti hatua kwa hatua.**

Utaratibu wa kusimamisha swala ya maiti ni kama ifuatavyo;

a) Maiti iwekwe mbele.

b) Imamu asimame katikati ya mwili wa maiti ikiwa maiti ni ya kike, na usawa wa mabega kama maiti ni ya kiume.

c) Maamuma watasimama kwenye mistari (safu) kwa idadi ya witiri; 1, 3, 5, n.k.

d) Baada ya hapo swala itaanza na kuendelea kama ifuatavyo:

i. Nia - ambayo ni kukusudia moyoni.

ii. Kuleta takbira ya kwanza; kwa kusema, “Allaah Akbar”

iii. Imamu na maamuma watasoma suratul-Faatiha – kimya kimya.

iv. Imamu ataleta Takbira ya Pili kisha maamuma – kimya kimya kwa maamuma na si lazima kuinua mikono wao.

v. Kumswalia Mtume (s.a.w) kama ilivyo katika Tahiyyatu, wote – kimya kimya.

vi. Imamu ataleta takbira ya Tatu kisha maamuma- kama walivyofanya awali.

vii. Wote kumuombea maiti dua kimya kimya, ikiwemo:

"Allaahumma ghfir lihayyinaa wamaayyitinaa washaahidinaa waghaaibinaa waswaaghirinaa wakaabirinaa wadhakirnaa waunthaanaa. Allaahumma man ahyaytahuu minnaa faahyi 'alal Islaam. Waman tawaffaytahuu minnaa tawaffahuu 'alal Imaani. Allaahumma laa tahirimnaa ajirahuu walaa taftinaa ba'adahuu"

Tafsiri:

"Ewe Allah tusamehe sisi, na maiti wetu, na mashahidi, na wasiokuwepo miongoni wetu, vijana wadogo miongoni mwetu na wakubwa miongoni mwetu, wanamume wetu, na wanawake wetu. Ewe Allah, yeyote yule miongoni mwetu utakayemewezesha kuishi, mjaalie aishi katika Kiislamu na yeyote miongoni mwetu utakayemfisha, mfishe katika Imani (ya Kiislamu). Ewe Allah, usitukatishe ujira kutoka kwake na wala usitufitinishe baada yake."

- Au kwa kifupi tuweza kumuombea maiti kama ifuatavyo;

"Allaahumma ghfir lahuu warhamhuu wa-afihii wa-afu-anhu"

Tafsiri:

"Ewe Allah, Mghufirilie na Umrehemu".

viii. Imamu ataleta Takbira ya nne na maamuma kufuatihia kama awali.

ix. Wote watawaombea waislamu dua – (pia si lazima kuleta dua hii).

Rejea Qur'an (59:10).

x. Imamu kutoa salaam na maamuma kufuatishia bila kutoa sauti kama ilivyo kwenye swala ya kawaida kwa kusema;

"Assalaamu 'alaykum Warahmatullaah (Wabarakaatuh)"

Tafsiri:

"Amani iwe juu yenu na Rehema za Allah na Baraka zake".

4. Kuzika.

- **Kusindikiza jeneza.**
  - Waislamu (watu) wataongozana nayo mpaka kaburini kimya kimya.
  - Jeneza lisitanguliwe na watu (msafara).
  - Haitakiwi watu kukaa kabla ya jeneza kukalishwa chini.

- **Kaburi.**
  - Kaburi liwe pana na kina cha kutosha, mtu kuweza kusimama na kunyoosha mkono kama kuna uwezekano.
  - Kisha lichimbwe shimo dogo (mwana ndani) upande wa Qibla ndani ya kaburi.
  - Urefu na ukubwa wa kaburi unategemea na ukubwa wa maiti.

- **Namna ya Kuzika hatua kwa hatua.**

a) Waingie watu kaburini kwa idadi ya witiri; 3, 5, 7, n.k.

b) Jeneza liwekwe upande wa kaburi itakapokuwa miguu ya maiti.

c) Maiti itolewe na kutanguliza kichwa kuelekea kaburini.

d) Wapokeaji kaburini watamuweka magotini mwao ili kufungua kamba kichwani, tumboni na miguuni. Pia watafunua shavu la kulia ili liguse ardhini (mchanga) atakapolazwa ndani ya mwana-ndani.

e) Maiti italazwa katika mwana-ndani kwa ubavu wa kulia na kuelekezwa Qibla. Wakati wa kuilaza ni sunnah kusema,

Kama ilivyosimuliwa na Ibn Umar (r.a) kuwa, Mtume (s.a.w) alipokuwa akizika alikuwa akisema:

"Bismillaah wabilahi wa'alaa millati Rasuulullaahi"

Tafsiri:

"Kwa jina la Allah na kwa uwezo wa Allah na kwa mujibu wa mwenendo wa Mtume wa Allah." (Ahmad, Tirmidh, Ibn Majah).

f) Maiti ipindishwe miguuni na kichwani ili uso na miguu iweze kugusa kuta za mwana-ndani. Kifua, tumbo na sehemu za katikati zibinuliwe nyuma kidogo.

g) Maiti iwekewe mawe au udongo nyuma ya kichwa na miguu isibinuke. Pia ni sunnah kusoma aya za Qur'an (2:1-5) au (2:285-286).

h) Baada ya maiti kulazwa na kusomewa aya hizi, ifunikwe kwa ubao na kama kuna matundu ya kupitisha udongo pazibwe kwa majani.

i) Kabla kaburi halijafunikwa, vitupiwe viganja vitatu vya udongo, na kila tupo unasoma aya ya Qur'an (20:55).

- **Tupo la 1:** *"Min-haa khalaq-naakum"* – Kutokana na hii (ardhi) tumekuumbeni.
- **Tupo la 2:** *"Wa fiyhaa nughiydukum"* – Na humo (katika ardhi) tutakurudisheni.
- **Tupo la 3:** *"Wa min-haa nukhrjukum taaratan-ukhraa"* – Na humo (katika ardhi) tutakutoweni mara nyingine.

j) Kaburi lijazwe udongo mpaka lijae na kuinuliwa kiasi cha shiburi moja na kuwekewa alama miguuni na kichwani au kupanda miti mibichi.

- Ni vizuri kumiminia maji juu yake ili kuepusha vumbi kupeperushwa na upepo.
- Ni haramu kujengea kaburi kwa namna yeyote ile, kukaa juu yake, kuwasha taa juu yake na kuielekea wakati wa kuswali.

> *'Jabir (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amekataza kuyajengea makaburi au kuyajengea nyumba juu yake au kukaa juu yake'.* (Muslim)

Abu Marsad Al-ghafariyyi ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema:

"Msikae juu ya makaburi na wala msiswali kwa kuyaelekea."

(Muslim)

- Baada ya kuzika Mtume (s.a.w) alikuwa akisimama na kusema:

"*Muombeeni msamaha ndugu yenu na muombeeni awe na kauli thabiti kwani sasa anaulizwa"*

- Ni sunnah baada ya mazishi kuwapa mikono wafiwa na kuwausia subira Rejea Qur'an (2:155-156).
- Pia haifai kusema (kusengenya) mabaya ya marehemu.

Zoezi la 3.

1. Bainisha mambo manne ya msingi kufanyiwa muislamu mara tu baada ya kufa.
2. Bainisha tofauti kati ya sanda ya;
   (a) Maiti ya mwanamke.
   (b) Maiti ya mwanaume.
   (c) Maiti ya toto.
3. (a) Taja nguzo za kuosha maiti.
   (b) Taja sehemu zinazofaa kutumika katika kuoshea maiti.
   (c) Ni zipi sifa za muosha maiti?

4. Eleza hatua kwa hatua namna ya kumuosha maiti wa Kiislamu.
5. Ni mambo gani maiti ya shahidi haitakiwi kufanyiwa? Taja mambo matatu.
6. Fafanua ni kwa vipi unaweza kuandaa sanda ya maiti wa kike na kumkafini.
7. Taja tofauti kati ya swala ya kumswalia maiti na swala ya kawaida.
8. (a) Ni yapi masharti ya kuswaliwa maiti wa Kiislamu?
   (b) Orodhesha nguzo za swala ya maiti.
9. (a) Eleza hatua kwa hatua namna kutekeleza swala ya maiti.
   (b) Taja mambo manne yaliyoharamishwa kufanyiwa kaburi.

4.0 NGUZO ZA UISLAMU

4.1 Shahada.

- **Tafsiri na Maana ya Shahada.**
  - **Shahada ya kwanza.**

    "*Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah"*

    - ***Sifa (tabia) za mtu aliyetoa Shahada ya Kwanza Kiutendaji:***
      - Hatamtii yeyote katika maisha yake ya kila siku ila Allah peke yake.
      - Hatamuogopa, hatamtegemea na hatamuomba yeyote ila Allah.
      - Hatafuata mwongozo wowote ila ule wa Allah pekee.
      - Hatamshirikisha Allah (s.w) kwa chochote kile.
      - Atajipamba na sifa na tabia njema zilizoainishwa katika Qur'an na Sunnah.

  - **Shahada ya Pili.**

    "*Nashuhudia kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Allah"*

    - ***Sifa (tabia) za mtu aliyetoa shahada ya Pili Kiutendaji:***
      - Kumtii Mtume (s.a.w) kwa kufuata aliyoagiza na kuacha aliyokataza.
      - Kumuiga Mtume (s.a.w) katika mwenendo na tabia yake.
      - Kumfanya Mtume (s.a.w) kuwa hakimu wa mambo yetu yote.
      - Kuliendea lengo la kuletwa kwake la kuusimamisha Uislamu katika jamii.

4.2 Kusimamisha Swala za Sunnah.

- **Umuhimu wa Kusimamisha Swala za Sunnah.**

a) Kusimamisha swala za Sunnah ni kumtii na kumuiga Mtume (s.a.w).
Rejea Qur'an (33:21) na (3:31).

b) Hutupelekea kuwa Wacha-Mungu kwa njia nyepesi kupitia utii na kujikurubisha zaidi kwa Allah (s.w).

c) Hutupelekea kufikia lengo la swala kwa kujitakasa na mambo machafu na mavu. Rejea Qur'an (29:45).

d) Swala za Sunnah pia hujaziliza mapungufu ya swala za faradhi ambazo hazikuswaliwa kikamilifu kutokana na udhaifu wa kibinaadamu.

- **Aina za Swala za Sunnah.**

Rejea Kitabu cha 1, EDK, Shule za Sekondari, Uk. 150-165.
Swala za Sunnah ni nyingi, tutaangalia baadhi tu kama ifuatavyo:

i. Swala ya Maamkizi ya Msikiti.

- Huswaliwa rakaa mbili muda wowote mara tu muislamu aingiapo msikitini kabla ya kukaa.

ii. Swala za Qabiliyyah na Ba'adiyyah.

- Hizi huswaliwa kabla (Qabiliyyah) na Baada (Ba'adiyyah) ya swala za Faradh.
- Ziko aina mbili; 'Mu'akkadah' (zilizokokotezwa) na 'Ghairu Mu'akkadah' (Hazikukokotezwa).
  Rejea Kitabu cha 1, EDK, Shule za Sekondari, Uk. 152.

iii. Swala ya Witiri.

- Huswaliwa rakaa kwa idadi ya witiri; 1, 3, 5, 7, 9 na 11 katika theluthi ya mwisho wa usiku au mara tu baada ya swala ya Ishaa.
- Witiri imekokotezwa mwisho wa usiku zaidi na huambatanishwa kwa dua ya Qunuti katika rakaa ya mwisho.

iv. Swala ya Tahajjud (Qiyaamul-layl).

- Huswaliwa rakaa 8 usiku wa manane kwa rakaa mbili mbili na kumalia 3 za witiri na kutimia rakaa 11.
- Huswaliwa kwa kisimamo na kisomo kirefu cha Qur'an.
  Rejea Qur'an (17:79), (25:64), (39:9) na (73:1-4).

v. Swala ya Tarawehe (Qiyaamu Ramadhan).

- Ni swala ya kisimamo na Kisomo kirefu cha Qur'an, Juzuu 1 kila siku inayoswaliwa mwezi wa Ramadhani tu baada ya Ishaa au kabla ya swala ya Alfajir.
- Kuna hitilafu kwa idadi ya rakaa, kauli zinasema ni rakaa 8, 11, 20, 36, n.k.lakini yenye nguvu ni rakaa 8 na 3 za witiri na kuwa jumla rakaa 11.

vi. Swala ya Idil-Fitr na Al-Udhuhaa.

- Zote huswaliwa rakaa mbili, Idil-Fitr huswaliwa mwezi 1 Shawwal baada ya kumalizika funga ya mwezi wa Ramadhani.
- Idil-Al-Udhuhaa huswaliwa mwezi 10 Dhul-Hija baada ya kukamilika ibada ya Hija kila mwaka.

vii. Swalatudh-Dhuhaa.

- Huswaliwa kila siku baada ya Jua kupanda kiasi cha mita tatu kutoka kuchomoza kwake.
- Huswaliwa rakaa mbili mbili hadi kutimia nane, lakini kwa uchache huswaliwa rakaa mbili.

viii. Swalatul-Istikharah.

- Ni swala inayoswaliwa muda wowote kwa ajili ya kuomba msaada na mwongozo kwa Allah juu ya uamuzi au utatuzi wa jambo lolote zuri.

ix. Swala ya Kukidhi Haja.

- Ni swala inayoswaliwa muda wowote kwa ajili ya kuomba msaada au utatuzi wa tatizo lililotokea au unalohitajia.

x. Swalatut – Tawbah.

- Huswaliwa rakaa mbili muda wowote kwa ajili ya kutubia baada ya muislamu kufanya kosa.
  Rejea Qur'an (3:135-136).

xi. Swala ya Kupatwa kwa Jua na Mwezi.

- Huswaliwa kwa jamaa, rakaa mbili, rukuu mbili kwa kila rakaa moja. Huswaliwa kwa kisimamo na kisomo kirefu mpaka Kupatwa kuondoke.

xii. Swala ya Kuomba (Swalatul-Istisqaa).

- Ni swala ya rakaa mbili kwa ajili ya kuomba mvua baada ya kuzidi dhiki na ukame, kwa jamaa na uwanjani.
- Swala hii ina khutuba mbili na takbira kama inavyoswaliwa swala za Idi.

4.3 Kutoa Zakat na Sadaqat.

- **Maana ya Zakat:**

Kilugha: Maana yake ni utakaso (purification).
Rejea Qur'an (91:9), (9:103) na (87:14).

Kisheria: Maana yake ni sehemu ya mali (2.5% au $^{1}/_{40}$) ya tajiri anayotakiwa kutoa kuwapa wanaostahiki baada ya kufikia kiwango cha Nisaab.

Nisaab: Ni kiwango (kima) akifikia au kuzaidi muislamu, analazimika kutoa zakat.

- **Maana ya Sadaqat:**

  Kilugha: Neno *'sadaqat'* linatokana na neno *"sidiq"* lenye maana ya ukweli.

  Kisheria: Sadaqat maana yake ni mali au huduma inayotolewa kwa mtu yeyote anayohitajia.

- **Tofauti kati ya Zakat na Sadaqat.**

Na.	Zakat	Sadaqat
1.	Inahusiana na utoaji wa mali tu.	Inahusiana na utoaji wa mali na huduma.
2.	Ni faradhi (amri) tu kwa tajiri muislamu aliyefikia kiwango cha Nisaab.	Ni wajibu kwa kila mtu kadri ya uwezo wake pindi inapohitajika.
3.	Zakat hutolewa kwa kiwango maalumu (2.5% au $^{1}/_{40}$) cha mali inayojuzu kutolewa zaka.	Sadaqat haina kiwango maalumu. Kila muislamu atatoa kulingana na uwezo wake.
4.	Zakat hutolewa baada ya mwaka au mavuno.	Sadaqat haina muda maalumu wa kutoa.
5.	Zakat hustahiki kupewa Waislamu tu.	Hupewa mtu yeyote bila kujali dini au uwezo wake, bali kila anayehitajia.

- **Umuhimu na Msisitizo wa Zakat na Sadakat katika Uislamu.**

  i. Zakat ni nguzo ya tatu ya Uislamu.

  ii. Kutoa zakat na Sadaka ni amri ya Mwenyezi Mungu (s.w).
  Rejea Qur'an (14:31) na (2:254).

  iii. Kutoa Zakat ndio kitambulisho cha Uislamu na Ucha-Mungu wa mtu.
  Rejea Qur'an (9:11) na (2:2-3).

iv. Kutoa Zakat na sadaka ni sababu ya mtu kufaulu Duniani na Akhera.
Rejea Qur'an (2:2-3), (23:1-4), (22:34-45) na (2:262,274).

v. Kutotoa Zakat na Sadaka ni sababu ya kuangamia mtu Duniani na Akhera.
Rejea Qur'an (9:34-35), (92:8-10) na (3:180).

- **Masharti ya Utoaji wa Zakat na Sadaqat.**

(a) Kutoa vilivyo halali.
(b) Kutoa vilivyo vizuri.
(c) Kutoa kwa kati na kati.
(d) Kuwapa wanaostahiki.
(e) Kujiepusha na ria na kufuatilia kwa masimbulizi.

(a) Kutoa Vilivyo halali.

- Mali ya halali na iliyochumwa kwa njia ya halali ndio inayofaa kutolewa Zakat ua Sadaqat. Mali ya haramu au iliyochumwa kwa njia ya haramu haikubaliki.
Rejea Qur'an (4:10), (23:51) na (2:172).

(b) Kutoa Vilivyo vizuri.

- Ni kutoa kile ukipendacho kwa dhati na ndio zina malipo makubwa kwa Allah.
Rejea Qur'an (2:267) na (3:92).

(c) Kutoa kwa kati na kati.

- Ni kutoa kwa kuzingatia kipimo (kiasi) ambacho hakiwezi kukuathiri katika matumizi ya maisha yako na familia pia.
Rejea Qur'an (2:219) na (17:29).

(d) Kujiepusha na ria na masimbulizi.

- Ni kutoa mali au huduma kwa ajili ya Allah pasina kujionyesha na kufuatilia kwa masimbulizi.
Rejea Qur'an (2:264), (2:271) na (2:274).

(e) Kuwapa Wanaostahiki.

- Zakat au Sadaqat hutolewa kupewa watu maalumu wanaohitajia, wenye matatizo na zikitolewa kwa asiyestahiki, huwa ni dhuluma.
  Rejea Qur'an (9:60).

- **Wanaostahiki kupewa Zakat.**

Kwa mujibu wa Qur'an (9:60) na (2:273), wanaostahiki kupewa Zakat ni waislamu tu katika makundi yafuatayo;

i. Fukara.

- Ni kundi la wale wasiojiweza kwa chochote cha kumudu maisha yao kabisa ya kila siku bila kusaidiwa.

ii. Maskini.

- Ni wale wasio na uwezo wa kupata mahitaji yao ya msingi ya kimaisha ila wana uwezo wa kujikimu kwa kiasi fulani tu.

iii. Wanaozitumikia (Al-A'miliina A'laihaa).

- Ni wale wote wanaozikusanya na kuzigawanya kwa wanaohusika bila kujali uwezo wao.

iv. Wanaotiwa nguvu nyoyo zao juu ya Uislamu.

- Ni wale walioingia katika Uislamu karibuni na wanahitajika kuimarishwa imani zao juu ya Uislamu.

v. Kuwakomboa Watumwa (Fir-riqaabu).

- Ni kuwakomboa au kuwanunua watumwa au watu wote wanaoishi chini ya miliki ya watu (mabwana) na kuwaachia huru.

vi. ***Kuwasaidia wanaodaiwa kulipa madeni yao.***

- Ni kuwalipia waislamu madeni yao waliokopa ili kujikimu kimaisha lakini bila kukusudia wameshindwa kulipa deni zao.

vii. ***Kutumika Katika njia ya Allah (s.w).***

- Ni kutumika katika shughuli zote zinazopelekea kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

viii. ***Kuwasaidia Wasafiri walioharibikiwa njiani (Ibnis-sabiil).***

- Msafiri yeyote muislamu aliyeharibikiwa kwa kupoteza, kuibiwa au kuishiwa mali yake hata kama ni tajiri, ni wajibu kupewa zakat.

- **Wanaostahiki kupewa Sadaqat.**

Kwa mujibu wa Qur'an (4:36) na (51:9);

- Sadaqat hupewa wale wale wanaopewa Zakat lakini bila kiwango au muda maalumu au kufikia nisaab.

- Sadaqat hupewa mwanaadamu yeyote hata wasiokuwa Waislamu ikiwa tu ni mwenye kuhitajia.

- Kila muislamu anao uwezo wa kutoa sadaqat, kwani inahusika na kutoa mali, huduma, tabia nzuri, n.k.
  Rejea Qur'an (2:263).

- Pia haifai kurejesha sadaqat baada ya kuitoa.

  Rejea Hadith ya Umar (r.a); Kitabu cha 2; EDK. Uk. 80.

- **Mali zinazojuzu kutolewa zaka, Nisaab zake na Viwango vyake.**

  Rejea Jedwali lifuatalo na pia katika Kitabu cha 2; EDK, uk. 80-87.

Na.	Mali zinazojuzu kutolewa Zakat	Nisaab (Kiwango)	Kiasi (%)	Muda wa Kutoa
1.	***Mazao yote ya shambani.***	Wasaq 5 au kg 666 (Wasaq 1 = 133.5kg)	(a) Kg 66.6 au ½ wasaq kwa mazao ya maji ya mvua. (b) Kg 33.3 au ¼ wasaq kwa mazao yaliyomwagiliwa.	Baada ya mavuno
2.	***Wanyama wafugwao kwa ajili ya chakula:*** (a) Ngamia (b) Ng'ombe (c) Mbuzi (d) Kondoo (e) Kondoo au Mbuzi	 Ngamia 5 Ng'ombe 30 Mbuzi 40 Kondoo 40 Kondoo au Mbuzi 40	 Mbuzi 1 wa mwaka 1 Ndama 1 wa mwaka 1 Mbuzi 1 wa mwaka 1 Kondoo 1 wa mwaka 1 Kondoo au mbuzi 1 wa mwaka 1	Baada ya mwaka
3.	***Dhahabu na Vito***	Gram 82.5 au tola 7.5	2.5 % au $^1/_{40}$ ya thamani ya mali	Baada ya mwaka
4.	***Fedha na Vito***	Gram 577.5 au tola 52	2.5 % au $^1/_{40}$ ya thamani ya mali	Baada ya mwaka
5.	***Mali ya Biashara***	Sawa na thamani ya Nisaab ya Dhahabu au Fedha.	2.5 % au $^1/_{40}$ ya mali	Baada ya mwaka
6.	***Fedha taslimu***	Sawa na mali ya Biashara	2.5 % au $^1/_{40}$ ya fedha	Baada ya mwaka
7.	***Mali ya kuokota au kuchimbuliwa ardhini***	Haina	20 % au $^1/_5$ ya mali	Baada ya kuokotwa na kukosa mwenyewe au baada ya kuchimbuliwa.

4.4 Funga ya Ramadhani na zinginezo.

- **Funga ya mwezi wa Ramadhani.**

Maana ya swaumu (funga).

***Kilugha*:** Kujizuilia kufanya jambo lolote ulilolizoea kulifanya.

***Kisheria*:** Ni kujizuilia na kila chenye kufunguza kuanzia Alfajir ya kweli hadi kuzama jua.

- **Umuhimu wa funga ya Ramadhani.**
  - Funga ya mwezi wa Ramadhani ni nguzo ya nne katika Uislamu.
  - Kufunga mwezi wa Ramadhani ni utambulisho wa Uislamu wa mtu.
  - Kufunga mwezi wa Ramadhani ni amri ya Mwenyezi Mungu (s.w). Rejea Qur'an (2:183).
  - Kufunga mwezi wa Ramadhani ni utambulisho wa Ucha-Mungu wa mtu.
  - Kutofunga mwezi wa Ramadhani makusudi hupelekea kukosa msamaha.

- **Kwa nini funga imefaradhishwa mwezi wa Ramadhani?**
  - Ndio mwezi ambao Qur'an imeteremshwa.

- **Nguzo za funga ya Ramadhani na zinginezo.**
  i. ***Nia*** – ya funga ya faradh hunuiwa kabla ya Alfajir kuingia.
     - ya funga ya sunnah hunuiwa hata kabla ya kuingia adhuhuri.

  ii. ***Kujizuia na kila chenye kufungusha*** – kuanzia Alfajir ya kweli hadi magharibi.

- **Sunnah za funga ya Ramadhani.**
  i. Kula na kuchelewesha daku kukaribia Alfajir ya kweli. Rejea Qur'an (2:187).
  ii. Kufuturu mapema mara tu baada ya Jua kuzama.
  iii. Kuzidisha ukarimu zaidi wakati wa funga ya mwezi wa Ramadhani.

iv. Kuzidisha kuisoma Qur'an zaidi mwezi wa Ramadhani kama mwongozo wa maisha.
Rejea Qur'an (2:185) na (25:73).

v. Kusimamisha swala ya Tarawehe mwezi mzima wa Ramadhani.

vi. Kuutafuta usiku wa Lailatul-Qadri kwa kukaa itikaf kumi la mwisho wa funga Ramadhani.
Rejea Qur'an (97:1) na (44:3).

- **Miiko au mambo yanayoharibu (yanayobatilisha) funga.**

a) Kula au kunywa chochote kwa makusudi.
b) Kujitapisha kwa makusudi ukiwa umefunga.
c) Kupatwa na Hedhi au Nifasi kabla ya kuzama kwa Jua.
d) Kunuia kula au kunywa na hali umefunga.
e) Kufanya tendo la jimai (tendo la ndoa) kwa namna yeyote ile hali umefunga.
f) Kujitoa manii kwa makusudi mchana wa funga.

- **Mambo yanayodhaniwa yanaharibu funga lakini hayaharibu.**

i. Kula au kunywa bila kukusudia – kwa kusahau au kutwezwa nguvu.
ii. Kuoga wakati umefunga.
iii. Kutokwa na manii bila kukusudia – kwa kuota ndoto au namna nyingine.
iv. Kuamka na Janaba, Damu ya Hedhi au Nifasi ukiwa umefunga.
v. Kubusiana na kukumbatiana mume na mke wakiwa wamefunga.
vi. Kupiga mswaki, kusukutua au kupandisha maji puani.
vii. Kupaka wanja, manukato, mafuta, kuvukiza ubani au dawa ya macho.
viii. Kumeza usichoweza kujizuia nacho kama mate, kikohozi, kuingiwa na mdudu (kitu) ghafla hadi kooni, vumbi, n.k.
ix. Kupiga sindano isiyoongeza chakula mwilini kama itahitajika.
x. Kuumika au kutoa damu kwa mujibu wa Hadith;

"*Amehadithia Ibn Abbas (r.a) kwamba Mtume (s.a.w) aliumikwa akiwa katika 'Ihram' na pia akiwa amefunga.*"

(Ameipokea Bukhari)

- **Waislamu wanaolazimika kufunga.**

a) Wenye akili timamu – sifa hii ni kwa kukubalika kila ibada.
b) Waliofikia baleghe – waliofikia umri wa kutambuzi jema na baya.
c) Wenye afya – wasio na ugonjwa unaoathiri afya kama akifunga. Rejea Qur'an (2:184-185).
d) Wakazi wa mji - wasiokuwa safarini au wasiokwazika kufunga safarini.
e) Kama mwanamke asiwe katika Hedhi au Nifasi – Damu ya mwezi au uzazi.

- **Wenye ruhusa ya kutofunga Ramadhani.**

i. Wasio na akili timamu.
ii. Wasiofikia baleghe.
iii. Wagonjwa wenye maradhi ya kudumu.
iv. Wasafiri.
v. Kufikwa na Hedhi au Nifasi kwa mwanamke.

- **Funga za Sunnah.**

- Nia ya kufunga Sunnah inaweza kutiwa muda wowote ule kabla ya Adhuhuri iwapo mfungaji hakuonja chochote tangu Alfajir.
- Kuna hiari ya kuvunja funga ya Sunnah muda wowote ule pindi itakapobidi.

- **Umuhimu wa funga za sunnah.**

1. Ni kumtii na kumuiga Mtume (s.a.w).
2. Ni kujazilizia mapungufu ya funga ya faradhi.
3. Humuwezesha muumini kufikia lengo la funga (kuwa Wacha-Mungu).

- **Funga za Sunnah na namna ya kutekeleza.**

a) Kufunga siku tatu kila mwezi.

- Ni kufunga siku tatu mfululizo za mbalamwezi, mwezi 13, 14 na 15.

b) Kufunga ya siku ya Jumatatu na Al-khamisi.

- Jumatatu ni siku aliyozaliwa Mtume (s.a.w) na Al-khamisi ni siku kupandishwa amali za mja kwenda kwa Mola wake.

c) Kufunga siku sita za mwezi wa Shawwal.

- Ni kufunga sita mara baada ya mwezi wa Ramadhani kuisha.

d) Funga ya Arafa.

- Ni kufunga siku ya mwezi 9, Dhul-Hijj ambamo mahujaji wako katika kisimamo katika uwanja wa Arafa.

e) Funga ya Ashura.

- Ni kufunga siku ya mwezi 10, Muharram (mfungo nne). Ni siku aliyookolewa Nabii Musa na Bani Israil kutoka kwa utawala wa Firaun.

f) Funga katika mwezi Shaaban.

- Ni kufunga kwa wingi katika mwezi wa Shaaban bila ya kutimiza siku 30.

- **Funga za Kafara.**

- Ni funga anazolazimika muislamu kufunga ili ziwe kitubio au fidia baada ya kutenda kosa fulani.

- **Aina za funga za kafara.**

1. Kufunga miezi miwili mfululizo kwa muislamu aliyemuua mtu kwa bahati mbaya na akakosa mali ya kulipa fidia.
   Rejea Qur'an (4:92).

2. Kufunga miezi miwili mfululizo kwa muislamu aliyemsusa mkewe kwa kumfananisha na mama mzazi wake.
   Rejea Qur'an (58:1-4).

3. Kufunga siku tatu mfululizo kama kafara kwa muislamu aliyevunja kiapo.
   Rejea Qur'an (5:89).

4. Kufunga miezi miwili mfululizo kwa mume na mke waliofanya jimai (tendo la ndoa) mchana wa mwezi wa Ramadhani.

5. Kufunga kama kitubio cha muislamu aliyewinda na hali yuko katika Ihram.
   - Idadi ya siku inategemea na thamani ya kile alichokiua (alichokiwinda).
   - Kama hana uwezo wa kufunga, atatoa fidia ya mbuzi au kondoo.

   Rejea Qur'an (5:95).

6. Kufunga siku 10, tatu akiwa Makkah na 7 baada ya kurejea nyumbani kwa muislamu aliyevunja miiko ya Ihram.
   - Kama hana uwezo wa kufunga, atafidia kwa kuchinja mbuzi au kondoo.

   Rejea Qur'an (2:196).

- **Siku zilizoharamishwa kufunga Sunnah.**

  i. Siku ya Sikukuu ya Iddil-Fitri na Iddil-Hajj.
  - Ni haramu kufunga siku za Idd mbili hizi kwa namna yeyote ile.

  ii. Siku za Tashriiq.
  - Siku za tashriiq ni tarehe 11 – 13, mwezi wa Dhul-Hajj.

  iii. Siku ya shaka.
  - Ni siku ya tarehe 29 au 30 mwezi Shaaban kabla ya mwezi wa Ramadhan.

  iv. Siku ya Ijumaa.
  - Haifai kufunga siku ya Ijumaa tu, isipokuwa kwa aliyekuwa na tabia ya kufunga Sunnah na ikatokea funga ya sunnah ni siku ya Ijumaa.

4.5 Hijja na Umrah.

- **Maana ya Hijja**

Kilugha: Kuzuru au kutembelea mahali kwa lengo maalum.

Kisheria: Ni kuizuru Ka'abah, nyumba tukufu ya Makkah katika mwezi na siku maalum kwa kuzingatia masharti na nguzo zote za Hija.

- **Maana ya Umrah**

Kilugha: Ni kutembelea.

Kisheria: Ni kutembelea nyumba tukufu ya Ka'abah katika mwezi na siku yeyote kwa kuzingatia sharti na nguzo za Umrah.

- **Tofauti kati ya Hijjah na Umrah.**

Na.	Hijjah	Umrah
1.	Hijjah ni faradh kwa muislamu mwenye uwezo mara moja kwa maisha yake yote.	Umrah ni Sunnah iliyokokotezwa.
2.	Hijjah ina muda maalum, hufanywa katika mwezi na siku maalum.	Umrah haina muda maalum, hufanywa mwezi na siku yeyote.
3.	Hijjah huchukua muda mrefu na hufanyikia ndani na nje ya Makka – Muzdalifa, Arafa na Mina.	Umrah huchukua muda mfupi na hufanyikia ndani ya Makka kwa Kutufu, Kusai na Kunyoa tu.
4.	Ibada ya Hijjah ina matendo mengi	Ibada ya Umrah ina matendo machache.

- **Umuhimu na Nafasi ya Hijjah katika Uislamu.**

i. Hijjah ni nguzo ya tano katika Uislamu iliyofaradhishwa kwa waumini. Rejea Qur'an (3:97).

ii. Hijjah na Umrah ni ibada za hali ya juu na zenye malipo makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w).

iii. Kuacha ibada ya Hijjah kwa mwenye uwezo kwa kukusudia anastahiki adhabu mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w).
Rejea Qur'an (3:97).

iv. Kuhiji ni amri ya Mwenyezi Mungu (s.w) kwa waumini wenye uwezo wa kimali na afya.

- **Wanaowajibika kuhiji.**
  - Waislamu wenye sifa zifuatazo wanalazimika kuhiji;
    a) *Waliobaleghe* – Watoto wadogo hawawajibiki kuhiji hata kama wana uwezo, hata hivyo wanaruhusiwa chini ya uangalizi wa wazazi wao.

    b) *Wenye Akili timamu* – Asiye na akili timamu hawajibikiwi kwa ibada yeyote ile katika Uislamu.

    c) *Waungwana* – Wafungwa au watumwa hawawajibiki kwa Hijja mkapa watakapokuwa huru.

    d) *Wenye uwezo* – Waislamu wote wenye uwezo kimali na afya njema ni wajibu kutekeleza ibada ya Hijjah.

    e) *Wasio katika kizuizi* – Waliowekewa kizuizi au kuzuiliwa kwa sababu za kiusalama sio wajibu kwao kuhiji muda huo.

    f) *Wanawake waongozane na maharimu wao.*
       – Mwanamke mwenye uwezo atawajibika kuhiji iwapo ataongozana na

maharimu wake.

- **Mwenendo wa mwenye kunuia Hijja au Umrah.**
  - Ajiepushe na kauli na vitendo viovu na vichafu.
  - Azidishe kusoma Qur'an na kusimamisha swala za faradh kwa jamaa na kusimamisha swala za sunnah kwa wingi.
  - Kuomba msamaha na kutubu kikweli kweli kwa Allah (s.w).
  - Kujitahidi kujipamba na kila tabia njema na kuamiliana kwa wema na wanahajj wengine.
  - Ajitahidi kujumuika na wanahajj kutoka sehemu mbali mbali Ulimwenguni.
  - Ajiepushe na matamanio wanapokuwa katika mchanganyiko wa wanaume na wanawake katika Hijja.

- **Vituo vya Kunuia Hijja au Umrah.**
  - ***Miiqaat***, ni vituo vya kunuia Hijjah na Umrah.
  - Vituo vitano alivyoviweka Mtume (s.a.w) ni;

    (a) Zul-Hulaifa (*Bir-'Ali*).
    - Ni cha watu watokao Madinah, kiko kilometa 450 kutoka Makkah.

    (b) Juhfah (*Rabigh*).
    - Ni cha watu watokao Misri na Syria, kiko kilometa 187 kaskazini-magharibi ya Makkah.

    (c) Qurnul-Manaazil (*Sail*).
    - Ni kituo cha watu watokao Najd, kiko kilometa 94 mashariki ya Makkah.

    (d) Makkah.

- Ni kituo cha wakazi wa Makkah na wale wanao nuia Hija mwezi 8, Dhul-Hijah.

(e) Yalamlam.

- Ni kituo cha watu watokao Yemen, Afrika Mashaiki na Afrika Kusini, kiko kilometa 54 kusini-magharibi ya Makkah.

(f) Dhaaru-Iraq.

- Ni kituo cha watu kutoka Iraq, Iran, n.k., alichokiweka Khalifah Umar Ibn Khatwaab (r.a) wakati wa ukhalifah wake.
- Kiko kilometa 94 kaskazini –mashariki ya Makkah.

(g) Jiddah.

- Ni kituo cha wasafiri wa ndege, kiko kilometa 72 kusini ya Makkah.

- **Yaliyoharamishwa kwa mwenye kuwa katika Ihram.**

- Kufanya jimai (tendo la ndoa), kubusu, kukumbatiana au kufanya ushawishi wowote wa kimapenzi kati ya mume na mke.

- Kusema au kutenda mambo machafu na maovu.
  Rejea Qur'an (2:197).

- Kunyoa nywele, kukata kucha, au kupunguza sehemu yeyote ya mwili isipokuwa kwa udhuru, kama matibabu, n.k.

- Kuoa, kuolewa, kutoa posa au kufanya mipango ya ndoa.
- Kujipaka manukato au kuvaa nguo zenye kuvutia.
- Kuvaa nguo iliyoshonwa na kufunika kichwa kwa wanaume.
- Kufunika uso na viganja vya mikono kwa wanawake kwa kuvaa gloves.

- Kuvaa viatu vya kufunika miguu na kuvaa soksi.
- Kuwinda au kusaidia kuwinda hata kwa kuonyesha mnyama anayewindwa.
- Kula nyama iliyowindwa au iliyopatikana kwa msaada wa mtu aliyekuwa katika Ihram.
- Kula mayai ya ndege waliopatikana kwa kuwindwa.

- **Aina za Hijjah.**
  - Kuna aina kuu tatu za Hijah ambazo Hajj ana uhuru wa kuchagua kulingana na uwezo wake.

  a) *Ifraad*.
     - Ni aina ya Hijja amapo Hajj anavaa Ihram kwa nia ya kufanya Hijjah tu bila ya Umrah.
     - Huanza kwa Talbiya; ***"Allaahumma labbaykal-Hijja"*** *– 'Nimeitika kwa Hijjah'*
     - Hajj huvaa Ihram mpaka amalize matendo yote ya Hija mwezi 10, Dhul-Hijjah.
     - Hajj halazimiki kuchinja siku ya mwezi 10, Dhul-Hijah.

  b) *Qiran*.
     - Ni aina ya Hija ambapo Hajj hunuia kufanya Hija na Umrah pamoja.
     - Hajj huitika kwa Talbiya; ***"Allaahumma labbaykal-Hijja wal-Umrata"*** *– 'Nimeitika kwa Hijjah na Umrah.'*
     - Hajj huwa katika Ihram mpaka alenge mawe minara mitatu, atufu Tawaful-Ifaadha na kunyoa mwezi 10, Dhul-Hijjah.
     - Hajj analazimika kuchinja mnyama.
     - Aina hii ya Hija hufanywa na wakazi wa Makka na wale waliokuja na wanyama.

c) *Tamattu.*

- Ni aina ya Hijah ambapo Hajj hunuia kufanya Umrah tu, kwa kuitika; ***"Allaahumma labbaykal-Umrah"*** *– 'Nimeitika kwa Umrah.'*

- Hajj huvua Ihram baada ya kufanya matendo yote ya Umrah na kunyoa na kuwa huru na miiko ya Ihram.

- Hajj huvaa tena Ihram siku ya mwezi 8, Dhul-Hija na kuitika; ***"Allaahumma labbaykal-Hijjah"*** *– 'Nimeitika kwa Hijjah.'*

- Hajj atavua tena Ihram baada ya kutupa mawe na kunyoa mwezi 10, Dhul-Hija.
- Hajj atalazimika kuchinja mnyama siku ya mwezi 10, Dhul-Hija kwa kununua mnyama kama hakuja nayo. Qur'an (2:196).

- Aina hii ya Hija ni bora na nafuu kwa wanaotoka mbali na hawana wanyama wa kuchinja.

- **Matendo ya Hija na Umrah.**

1. Ihram na Nia ya Hija na Umrah.

- Ihram huvaliwa nyumbani au katika vituo (miiqaat) vya kunuia Hija na Umrah.
- Nia ya Hija na Umrah hufanyika katika miiqaat baada ya kuswali rakaa mbili. Rejea Qur'an (22:27-28).

2. Talbiya.

- Ni maneno ya kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu (s.w) kulingana na aina ya Hija anayokusudia Hajj.
- Maneno haya huanzia miiqaat hadi kufikia Ka'abah.

3. **Tawafu.**

- Ni kitendo cha kuizunguka Ka'abah mara saba kuanzia kona ya jiwe jeusi (Hajaral-aswad) kwa kulibusu au kuligusa kwa kidole au kuashiria.

- Mzunguko hufanywa kwa mwelekeo wa kinyume na mwendo wa saa (Ant-clockwise direction).

- Tawafu hufanywa mtu akiwa katika twahara, Hajj akikatisha tawafu kwa udhuru wowote ule, ataanzia pale alipokatishia.

- **Aina za Tawafu.**

a) Tawaful-Quduum.

- Ni tawafu (ya Umrah) inayofanywa mara tu baada ya kuingia Makkah kwa ajili ya Hija au Umrah.

- Wanaume huvalia vipande viwili vya shuka, moja kiunoni na nyingine hufungwa lubega kwa kuacha wazi bega la kushoto (*Iztibaa*).

- Wwanaume hutembea mwendo wa matiti (jogging) (kukimbia - Ramal) mizunguko ya tatu ya mwanzo na minne iliyobaki kawaida.

b) Tawaful – Ifadha (Tawafu ya Nguzo).

- Ni tawafu ya Hija inayofanywa siku ya mwezi 10, Dhul-Hija. Pia inaitwa Tawafuz-Ziyaara.
- Hakuna Iztibaa na Ramal katika tawafu hii.

c) Tawaful-Widaa.

- Ni tawafu ya kuaga inayofanyika baada ya kumaliza Umrah au Hija tayari kurejea majumbani mwao.

4. Kusa'i.

- Ni kitendo cha kutembea mara saba baina ya vilima viwili vya 'Saffa' na 'Marwa' kwa kuanzia 'Saffa' na kuishia 'Marwa.'
  Rejea Qur'an (2:158).

- Aliyenuia Umra tu, baada ya kusai atanyoa na kuwa huru na masharti ya Ihram.
- Walionuia Hija ya Qiran na Ifrad watabakia katika Ihram na hawatanyoa.

5. Siku ya Tarwiya (mwezi 8, Dhul-Hija).

- Ni siku ya mwezi 8, Dhul-Hija ambapo Mahujaji huondoka Makka kuelekea Mina kabla ya Adhuhuri.

- Swala zote tano huswaliwa Mina kwa wakati wake, Adhuhuri hadi Alfajir ya mwezi 9, Dhul-Hija kwa kuzifupisha lakini bila kuzikusanya mbili mbili.

6. Siku ya Arafa (mwezi 9, Dhul-Hija).

- Arafa ni bonde lililo baina ya vilima vitatu.
- Siku ya Arafa ni mwezi 9, Dhul-Hija ambapo Mahujaji husimama (hukaa) katika uwanja wa Arafa na kuomba dua mbali mbali na maghufira kuanzia Adhuhuri hadi kukaribia kuzama jua.

- Kabla ya maghribi kuingia, Mahujaji huondoka Arafa na kuelekea Muzdalifa.
  Rejea Qur'an (2:199).

7. Kulala Muzdalifa.

- Muzdalifa ni kitongoji kilichopo baina ya Arafa na Minah.
- Mahujaji huswali Magharib na Isha na kulala humo na kuswali Alfajir kabla ya kuelekea Minah.
- Wakiwa njiani kuelekea Minah, Mahujaji huokota vijiwe saba kwa ajili ya kulenga mnara mkubwa watakapofika Minah.
  Rejea Qur'an (2:198).

8. Siku ya kuchinja (mwezi 10, Dhul-Hija).

- Matendo ya siku ya kuchinja ni pamoja na;
  i. Kutupa mawe kwenye mnara mkubwa – Jamatul-Aqaba.
  ii. Kuchinja mnyama kwa wenye kuhiji Hija ya Tamattu na Qiran.
  iii. Kunyoa kichwa kwa wanaume na kupunguza kwa wanawake.
  iv. Kutufu tawaful-ifadha (Tawafu ya Nguzo).

9. Siku za Tashriq (mwezi 11-13, Dhul-Hija).

- Ni siku za mwezi 11-13, Dhul-Hija.
- Mahujaji hukaa kambini Minah na kutupa vijiwe saba kila mnara katika minara mitatu pindi linapopinduka jua.
- Huswaliwa swala za faradh kwa wakati wake bila kuzikusanya, lakini kwa kuzipunguza rakaa.

10. Tawaful - Widaa.

- Ni tawafu ya kuaga baada ya Hajj kukamilisha matendo yote ya Hija au Umrah na tayari kurejea makwao.
- Tawafu hii haina '*Ramal'* na '*Iztibaa*.'. Rejea Qur'an (2:203).

- **Matendo (mambo) yanayobatilisha Hija pindi yasipotekelezwa.**

i. Nia au Ihram isipotekelezwa kwa kufuata masharti yake ipasavyo.
ii. Sai (kati ya Saffa na Marwa).
iii. Kuhudhuria katika uwanja wa Arafa mwezi 9, Dhul-Hija.
iv. Tawaful-Ifadha (Tawafu ya Nguzo).

- **Umuhimu wa siku ya Iddil-Haj na Sunnah ya kuchinja.**

- Ni siku ya kumshukuru na kumtaja sana Allah (s.w) kwani ndiye aliwezesha Ibada ya Hija kukamilika.
- Ni siku ya kujipumzisha baada ya ibada ngumu na misukosuko mingi.
- Ni siku ya kufurahi na kujumuika pamoja kutathmini utekelezaji wa ibada za Hija.
- Ni siku ya kuonyesha utayari wetu wa kujitoa muhanga kwa ajili ya kupigania Uislamu kwa kuchinja vile tulivyoruzukiwa.
- Ni kuiga na kufuata mila ya Baba yetu Nabii Ibrahim (a.s).

Zoezi la 4.

1. (a) Bainisha sifa za mtu aliyetoa shahada ya kweli.
   (b) Kwa nini ni umuhimu kusimamisha swala za Sunnah?
   (c) Taja swala tano za Sunnah zinazoswaliwa wakati wa matukio maalum zisizokuwa na muda maalum, kwa kueleza na aina ya tukio.
2. (a) Bainisha tofauti tano kati ya Zakat na Sadaqat.
   (b) Ainisha masharti ya utoaji wa Zakat na Sadaqat.
3. (a) Eleza maana ya maneno yafuatayo:
   (i) Nisaab (ii) Sadaqat (iii) Wassaq. (iv) Zakat
   (b) Kwa kurejea Qur'an (9:60), ni yapi makundi yanayostahiki kupewa Zakat?
4. Bainisha aina za mali zinazostahiki kutolewa Zakat, viwango vyake na muda kutoa.
5. (a) Taja mambo yanayobatilisha funga ya mtu.
   (b) (i) Nini maana ya 'swaumu' kilugha na kisheria?
   (ii) Taja nguzo za funga.

(c) Ni watu gani wanaoruhusiwa kutofunga mwezi wa Ramadhani?

(d) Sunnah zinazoambatana na funga ya Ramadhani ni;

(i) …… (ii) …… (iii) …… (iv)…… (v) ……

6. (a) Taja watu wanaolazimika kufunga mawezi wa Ramadhani

(b) Eleza aina za funga za kafara ambazo mfungaji analazimika kufunga miezi miwili mfululizo.

(c) Ni sababu zipi zinazopelekea mtu kufunga funga ya kafara?

7. (a) Ainisha aina za funga za Sunnah ulizojifunza.

(b) Orodhesha siku zilizoharamishwa muislamu kufunga Sunnah.

8. Eleza jinsi funga inavyomuandaa mfungaji kuwa Mcha-Mungu.

9. (a) Eleza maana ya neno;

(i) Hijja (ii) Umrah (iii) Miiqaat (iv) Tawafu (v) Ihram

(b) Bainisha tofauti kati ya Hijja na Umrah.

(c) Ainisha vituo vya kunuia Hijjah au Umrah.

10. (a) Fafanua aina za Hijjah.

(b) Ni mambo yapi yasipotekelezwa Hijja hubatilika (huharibika)?

(c) Taja matendo katika ibada ya Hijja ambayo Hajj hulazimika kuwa twahara (kuwa na udhu).

5.0 QUR'AN

5.1 Kushuka Qur'an.

- **Hatua mbili kuu za kushuka Qur'an;**

i. Kushuka kwa jumla kutoka Lawhi-Mmahfuudh hadi mbingu ya Dunia.
ii. Kushuka kigodo kidogo kutoka mbingu ya Dunia kwenda kwa Mtume (s.a.w).

- Qur'an ilianza kushuka mnamo mwaka 610 A.D, Mtume (s.a.w) akiwa na umri wa miaka 40.
- Qur'an ilikamilika kushuka kwa muda wa miaka 23 sehemu kidogo kidogo.
  Rejea Qur'an (97:1), (2:185), (44:3).

▪ **Hekima ya Qur'an kushuka hatua kwa hatua;**

- Ni kujibu hoja mbali mbali zilizotolewa na zilihitajia majibu ya kiwahyi.
- Ni kuwezesha utekelezaji wa maamrisho yake kuwa rahisi au mwepesi.
- Ili iwe rahisi kuhifadhika katika mioyo ya maswahaba.

5.2 Kuhifadhiwa kwa Qur'an.

- Mtume (s.a.w) aliwaamrisha maswahaba wake kujifunza na kuifahamu Qur'an na kuihifadhi moyoni.

- Mtume (s.a.w) aliteuwa baadhi ya maswahaba kuiandika Qur'an ilipokuwa inashuka.
- Kuhifadhiwa kwa kusomwa mara kwa mara.
- Qur'an pia ilihifadhika kwa kusomwa mara kwa mara katika ibada za swala.

5.3 Mafunzo ya sura zilizochaguliwa.

▪ **Suratul-Lahab (111): Imeteremshwa Makka; Ina Aya Tano.**
Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

1. Imeangamia mikono ya Abulahab naye amekwisha angamia.
2. Haitamfaa mali yake wala alivyovichuma (watoto).
3. (Atakapokufa) Ataingia moto wenye muwako (mkubwa kabisa).
4. Na mkewe (ni) mchukuzi wa kuni (za fitina).
5. (Kana kwamba) Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (anayechukulia kuni za fitina).

Mafunzo ya sura kwa ufupi.

1. Binaadamu siku zote huamua kumkanusha Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kibri na jeuri.
2. Mali na watoto havina msaada wowote pindi inapokuja adhabu ya Mwenyezi Mungu (s.w).
3. Watu waovu na wenye kumuasi Mwenyezi Mungu (s.w) wana mwisho mbaya wa kuishia motoni.
4. Maadui wa Uislamu na waislamu siku zote hawakati tamaa katika kuzuilia watu kuingia na kuufuata Uislamu.
5. Uchochezi, fitina na uasi ni miongoni mwa makosa makubwa yenye kuangamiza.

- **Suratul-Nnasr (110): Imeteremshwa Madinah Ina Aya Tatu.**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

1. Itakapofika Nusura ya Mwenyezi Mungu na Kushinda.
2. Na ukawaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi.
3. Basi (hapo) mtakase Mola wako pamoja na kumsifu na umuombe magh'fira (msamaha) hakika Yeye ndiye apokeaye toba.

Mafunzo ya Sura kwa Ufupi.

1. Nusura na mafanikio hutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w) pekee.

2. Baada ya nusura na ushindi hatuna budi kumshukuru, kumtukuza na kumuomba msamaha Mwenyezi Mungu (s.w) bila ya kujivuna.
3. Katika kufanya juhudi, hatuna budi kuchunga na kutii ipasavyo maarisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.
4. Nusura na mafanikio ya kweli huja baada ya juhudi za dhati za kibinaadamu kufanyika na kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w) vilivyo.
5. Mafanikio ya kweli sio kujilimbikizia mali na anasa za dunia tu, bali ni kuipigania Dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) ipasavyo.

- **Suratul-Kaafiruun (109): Imeteremshwa Makkah, Ina Aya Sita.**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

1. Sema: Enyi Makafiri.
2. Siabudu mnachoabudu.
3. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.
4. Wala sitaabudu mnachoabudu.
5. Wala nyinyi hamtaabudu ninayemuabudu (mimi).
6. Nyinyi mna dini yenu na mimi nina dini yangu.

Mafunzo ya Sura kwa Ufupi.

1. Dini ni utaratibu wowote ule wa maisha anaoufuata mtu.
2. Kuna dini nyingi hapa Ulimwenguni, Ukafiri nao ni dini.
3. Hakuna uwezekano wa mwanaadamu kufuata dini (utaratibu wa maisha) za ya moja kwa wakati moja, Uislamu na mifumo mingine.
4. Waislamu wa kweli ni wale wasiochanganya haki na batili kwa kuwahofia makafiri.
5. Ni wajibu kuitangaza haki kwa wengine bila kuhofia chuki na uadui wao dhidi ujumbe uliowapa.

- **Suraul-Kawthar (108): Imeteremshwa Makka, Ina Aya Tatu.**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

1. Hakika tumekupa kheri nyingi.
2. Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili yake pia).
3. Hakika adui yako ndiye atakayekuwa mkiwa (atakatikiwa na kila kheri).

Mafunzo ya Sura kwa Ufupi.

1. Mafanikio hayapimwi kwa wingi wa mali na watoto, bali ni kuridhiwa na Mwenyezi Mungu (s.w).
2. Hakuna neema kubwa kama kujaaliwa kuupokea Uislamu, kuuelewa, kuufuata vilivyo na kuufikisha kwa wengine.
3. Hatuna budi kumuabudu Mwenyezi Mungu (s.w) peke yake ipasavyo na kufanya kila jambo kwa ajili yake tu.
4. Maadui na Wapinzani wa Uislamu ndiyo wenye kupata khasara na kufedheheka duniani na Akhera pia.
5. Ushindi na mafanikio hupatikana kwa waislamu baada ya kutii na kufuata maamrisho ya Uislamu vilivyo.

- **Suratul-Maaun (107): Imeteremshwa Makka, Ina Aya Saba.**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

1. Je, Unajua yule anayekadhibisha dini (asiyeamini malipo ya Akhera)?
2. Huyu ni yule anayemnyanyasa yatima.
3. Wala hajihimizi (yeye wala wengine katika) kuwalisha maskini.
4. Basi adhabu kali itawathubutikia wanaoswali.
5. Ambao wanapuuza (maamrisho ya) swala zao.
6. Ambao hufanya riyaa (ya kujionyesha kwa watu).
7. Nao hunyima misaada (midogomidogo kwa wanaohitajia).

Mafunzo ya Sura kwa Ufupi.

1. Imani katika Uislamu hudhihirishwa katika matendo ya mtu na sio kauli au maneno tu.
2. Kuwadhulumu, kuwasimanga au kuwatendea uovu wowote mayatima na wenye shida ni katika makosa makubwa.
3. Swala ni lazima itekelezwe kwa kuzingatia ipasavyo nguzo, sharti zake pamoja na khushui (unyenyekevu).
4. Kutenda jambo lolote kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu (s.w) ndio uhai wa ibada ya muumini.
5. Maisha ni jambo la kijamii ambalo linahitajia watu kuishi pamoja kwa kusaidiana inapobidi.
6. Muumini wa kweli ni yule aliyemwepesi kutoa misaada kwa wanaadamu wenzie na mwenye kujali matatizo ya wengine yanapowapata.

- **Suratul - Qureish (106): Imeteremshwa Makkah, Ina Aya Nne.**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

1. Ili kuwafanya Maqureish waendelee.
2. Waendelee na safari zao za wakati wa kusi (kwenda Yemen) na wakati wa kaskazi (kwenda Sham ndiyo maana tukajaalia jeshi la ndovu kushindwa).
3. Basi na wa muabudu Bwana wa Nyumba hii (Al-Kaaba).
4. Ambaye amewalisha (wakati wa) katika njaa na anawapa amani (wakati wa) katika khofu.

Mafunzo kwa Ufupi.

1. Kwa hakika anayelisha na kulinda ni Mwenyezi Mungu (s.w) peke yake.
2. Amani, Usalama na Ustawi wa kweli wa jamii hutokana na kushikamana na amri za Mwenyezi Mungu (s.w).
3. Shukrani za kweli kwa Mwenyezi Mungu (s.w) ni kumuabudu ipasavyo.
4. Maingiliano ya Mataifa kibiashara ni katika neema za Mwenyezi Mungu (s.w).

Zoezi la 5.

1. (a) Orodhesha majina matano ya Qur'an unayoyafahamu.
   (b) Kwa kutumia ushahidi wa aya, onyesha kuwa Qur'an ilishushwa katika usiku Mtukufu wenye cheo.
2. (a) Eleza hatua mbili za kushushwa Qur'an.
   (b) Fafanua hatua zilizotumika katika kuihifadhi Qur'an wakati Mtume (s.a.w).
3. Onyesha hekima ya Qur'an kushushwa kidogo kidogo na hatua kwa hatua.
4. Andika tafsiri ya Suratul-Lahab, kisha toa mafunzo yake kwa muhtasari.
5. 'Nusura ya Mwenyezi Mungu inapokuja watu huingia katika Uislamu makundi kwa makundi'. Toa ushahidi huu kwa kurejea historia ya Mtume (s.a.w) alipokuwa mji wa Makkah na Madinah.
6. Kwa kurejea Suratul-Kafiruun, eleza kwa ufupi mafunzo yatokanayo na sura hiyo.
7. *"Adhabu kali itawathubutikia wale wanao swali, (Wale) ambao wanapuuza swala zao....."* (107:4-5).
   Kwa mujibu wa aya hii, onyesha jinsi waislamu wa leo wanavyopuuza swala zao.

6.0 SUNNAH NA HADITH

6.1 Uandishi wa Hadith za Mtume (s.a.w).

I. Uandishi wa Hadith wakati wa Mtume (s.a.w).

- Hapakuwa na uandishi mkubwa wa Hadith wakati wa Mtume (s.a.w) kwa sababu zifuatazo;
    a) Mtume (s.a.w) mwenyewe alikuwepo, hivyo walimfuata kupata maelekezo yake na kuiga mwenendo wake.

    b) Kipindi hicho maswahaba walijishughulisha sana na uandishi, uifadhi na utekelezaji wa mafundisho wa Qur'an katika maisha yao yote.

    c) Mwanzo, Mtume (s.a.w) aliwakataza maswahaba wake kuandika Hadith ili wasijekuchanganya na aya za Qur'an.
        - Lakini hata alipowaruhusu hawakujishughulisha kuandika Hadith tena, kwani walizoea kutoandika.

    d) Kipindi hicho, Mtume (s.a.w) na maswahaba walijishughulisha zaidi katika kuusimamisha Uislamu na kuuhami na maadui.

II. Uandishi wa Hadith wakati wa Maswahaba wa Mtume (s.a.w) (11 A.H – 101 A.H).

- Kipindi hiki kilichukua karne moja tangu kufariki (kutawafu) Mtume (s.a.w) hadi kufariki swahaba wa mwisho.

- Uandishi wa Hadith kipindi hiki haukuwa mkubwa sana ambao haukutosheleza mahitajio ya Hadith wakati huo, ulikuwa uandishi wa aina mbili tu;
    a) Kitabu cha Hadith cha **'Al-Qatadaya'** cha Ali (r.a).
    b) **Juzuu (Pamphlet) ya Hadith** iliyoandikwa na Ibn Abbas (r.a).

- Katika kipindi hiki, haja ya uandishi wa Hadith ilijitokeza kwa sababu zifuatazo;
    i. Dola ya Kiislamu ilipanuka sana na ikawa kuna hitajio kubwa la kuiendesha kwa mujibu wa mafundisho ya Qur'an na ya Hadith pia.

ii. Makhalifah wanne waongofu, waliongoza Dola ya Kiislamu kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah kwa kutoa hukumu mbali mbali.

iii. Kuzuka ugomvi baina ya Ali (r.a) na Muawiya (r.a) na waislamu kugawanyika makundi matatu na Hadith kutumika vibaya kulingana na matashi ya kila kundi.

iv. Kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu na kuibuka tawala za Kifalme, hivyo zilizuka hadith za uongo.

III. Uandishi wa Hadith Wakati wa Tabi'ina (wafuasi wa maswahaba),

(101 A.H – 200 A.H).

- Ni karne ya pili ambapo wanazuoni wengi walijitokeza waliojizatiti katika kazi ya ukusanyaji wa Hadith kutoka vituo mbali mbali vya elimu.

- Vituo mashuhuri vya elimu kipindi hicho vilikuwa; Madinah, Makkah, Baghdad, Basra, Khurasan na Kufa.

- Pia ni kipindi hiki ambapo walitokea maimamu wanne mashuhuri wa Fiqh ambao ni;

1. Imamu Abu Hanifa Al-Nu'man bin Thabit (80 – 150A.H).

- Mwanachuoni wa Qur'an na Hadith katika mji wa Kufa, Iraq.
- Alitoa Fat'wa za kifiq kwa kutumia Qur'an, Hadith na Ijmaa.
- Hakuandika kitabu chochote.

2. Imam Malik bin Anas (95 – 179 A.H).

- Mwanachuoni mcha-Mungu wa mji wa Madinah.

- Aliandika kitabu mashuhuri cha Hadith kiitwacho, "***Al-Muwatta***" kilichotegemewa na umma wa waislamu katika ibada maalum tu.
- Alifutu mas'ala ya Uislamu kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah tu.

3. Imam Muhammad bin Idris Al-Shafii (150 – 204 A.H).

- Mwanachuoni mkubwa wa sheria za Kiislamu aliyezaliwa Gaza, Palestina.
- Imam Malik bin Anas ni miongoni mwa walimu wake.
- Alitoa fat'wa kwa mujibu wa Qur'an, Hadith na Ijmaa (na Qiyaas pia).
- Hakuandika kitabu chochote cha Hadith.

4. Imam Ahmad bin Muhammad bin Hambal (164 – 241 A.H).

- Mwanachuoni mkubwa wa Fiqh na elimu ya Hadith aliyezaliwa mji wa Baghdad, Iraq.
- Imam Shafii alikuwa mwalimu wake.
- Imam Ahmad alitoa fat'wa tofauti na mwalimu wake, Imam Shafii lakini waliheshimiana sana.
- Aliandika kitabu cha Hadith kiitwacho, ***"Isnad ya Ibn Hambal"*** kilichokusanya zaidi ya Hadith 30,000.

- Pamoja na jitihada kubwa za ukusanyaji wa Hadith, wanazuoni hawa waliandika vitabu mashuhuri viwili tu;
  1) ***Al-Muwatta*** cha Imam Malik bin Anas.
  2) Isnad ya Ibn Hambal ***(Musnad Ahmad)*** cha Imam Ahmad bin Hambal.

IV. Uandishi wa Hadith Wakati wa Tabi'i Tabi'ina (wafuasi wa wafuasi wa maswahaba, 201 – 300 A.H).

- Pamoja na uandishi wa Hadith katika karne ya pili, bado kulikuwa na hitajio kubwa la mafunzo ya hadith katika kuendeshea maisha ya kila siku.

- Uandishi wa Hadith karne ya tatu, ulihusika na ukusanyaji wa Hadith kuhusu nyanja zote za maisha ya jamii.

- Wanachuoni pamoja na kukusanya Hadith nyingi muda huo, walikuwa makini mno katika kuchambua usahihi wa Hadith kwa kuzingatia;

    1) Tabia na mwenendo wa kila msimulizi (mpokezi) wa Hadith hiyo.
    2) Usahihi wa Matin ya Hadith hiyo.

- Ni kipindi hiki wanazuoni sita walijitokeza waliokusanya na kuchambua kwa umakini mkubwa Hadith sahihi na kuziandika katika vitabu sita mashuhuri kama, ***"Sahihu Sitta"*** ambavyo ni;

1. Sahihi Al-Bukhari.

- Ni kitabu cha *Muhammad bin Ismail Abu Abdallah Al-Ju'fi* – mashuhuri kama ***Imam Bukhari*** wa mji wa Bukhara, Urusi (194 A.H/810 A.D – 256 A.H/870 A.D).

- Alikusanya Hadith 600,000 na kuhifadhi 200,000 na alihakiki na kuandika Hadith 7,275 tu katika kitabu chake.

- Kitabu chake ndio namba moja kwa usahihi wa Hadith, mashuhuri kwa jina la "***Al-Jami'u Al-Sahihi"*** au "***Sahihi Bukhari".***

2. Sahihi Muslim.

- Ni kitabu cha *Abu Husain Muslim bin Al-Hajjaj* mashuhuri – *Imam Muslim* wa mji wa Misabur, (202 A.H/818A.D – 261 A.H/875 A.D).

- Alikusanya Hadith 300,000 na alizohakiki na kuziandika katika kitabu chake ni 9,200 tu.

- Kitabu chake ni namba mbili kwa usahihi wa Hadith, mashuhuri kwa jina la "Sahihi Muslim"

3. ***Sunan Abu Daud.***

   - Ni kitabu cha hadith cha *Imam Abu Daud* (203 – 275 A.H).
   - Alikusanya Hadith 500,000 na alizohakiki na kuziandika ni 4,800 katika kitabu chake kiitwacho, ***"Sunan Abi Daud".***

4. ***Jami'u at-Tirmidh.***

   - Ni kitabu cha Hadith cha *Abu Isa Muhammad bin Issa bin Sarwa bin Shaddad,* mashuhuri kama *Imam At-Tirmidh* (209 – 279 A.H).
   - Aliandika kitabu cha Hadith mashuhuri kwa jina la, ***"Jami'u".***

5. ***Sunnah (Sunan) Ibn Majah.***

   - Ni kitabu cha Hadith cha *Muhammad bin Yazid* – mashuhuri kwa jina la *Imam Ibn Majah* (209 A.H – 295 A.H).
   - Aliandika cha Hadith mashuhuri kama, ***"Sunanu Ibn Majah"*** au "Sunnah Ibn Majah".

6. ***Sunnah (Sunan) An-Nasai.***

   - Ni kitabu cha Hadith cha *Abu Abdur-Rahman Ahmad bin An-Nasai* – mashuhuri kwa jina la, *Imam An-Nasai* (214 – 303 A.H).
   - Aliandika kitabu cha Hadith mashuhuri kama, ***"Sunan An-Nasai"*** au "Sunnah An-Nasai".

- Hadith za Bukhari na Muslim ndio ***daraja la kwanza kwa usahihi*** na za Maimam Abu Daud, Tirmidh, Ibn Majah na An-Nasai ni ***daraja la pili kwa usahihi***.

6.2 Uchambuzi wa Hadith za Mtume (s.a.w).

- **Matin na Isnad ya Hadith.**

- ***Matin***: Ni kauli (maneno) aliyoyasema Mtume (s.a.w) au matendo yake au yale aliyoyaridhia.
- ***Isnad***: Ni msururu wa wapokezi (wasimulizi) wa hadith kuanzia kwa Mtume hadi kwa msimuliaji wa hadith hiyo.

Mfano wa Matin na Isnad ya Hadith;

Amesimulia Abdallah toka kwa Malik toka Abu Hurairah ambaye ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema, *"Mlaji mwenye ……..ni sawa na ....."* (Tirmidh).

Isnad, ni Wapokezi (wasimulizi) wa Hadith; Abdallah, Malik na Abu Hurairah.

Matin, ni Kauli ya Mtume (s.a.w); "Mlaji mwenye…..ni sawa na ….".

Maneno yaliyo katika, **"……."** ndio Matin ya Hadith.

- ***Riwaya***: ni Matin moja iliyosimuliwa na misururu tofauti ya wapokezi wa Hadith.

Rawi (**Rawahu**): ni mkusanyaji, mwandishi, mpokezi wa Hadith.

- **Uhakiki wa Hadith za Mtume (s.a.w).**

- Hadith za Mtume (s.a.w) zilihakikiwa kupitia njia mbili kuu;

a) Uhakiki wa Isnad.

- Ulizingatia na kuchambua msururu wa wapokezi (wasimulizi) wa Hadith kwa kuangalia historia yake, ucha-Mungu wake, tabia yake, n.k.

b) Uhakiki wa Matin.

- Ulizingatia usahihi wa Hadith kupitia masharti na vigezo vifuatavyo;
  i. Isipingane na aya za Qur'an.
  ii. Isipingane na Hadith nyingine iliyothibitika kuwa ni sahihi.
  iii. Isimzulie Mtume (s.a.w) kufanya jambo ambalo ni kinyume na Uislamu.
  iv. Isipingane na hakika au uhalisia (fact).

v. Isipingane na hakika au uhalisia wa kihistoria (historical fact).

vi. Isiwe na maneno ya uwongo ndani yake.

vii. Isiwe inaahidi adhabu kubwa sana kwa kosa dogo sana na kuahidi malipo makubwa sana kwa tendo (amali) dogo sana.

- **Aina za Hadith.**
  - Kuna aina kuu mbili za Hadith.

a) Hadith an-Nabawiyyi.

- Ni Hadith ambayo matin yake ni kauli ya Mtume (s.a.w) mwenyewe katika kuelezea jambo.
- Huanza kwa kauli; amesema Mtume wa Allah, "……"

b) Hadith Qudusiyyi.

- Ni Hadith ambayo matin yake (msimulizi wake) ni kauli ya Mtume (s.a.w) kama alivyoipokea kutoka kwa Allah (s.w) nje ya Qur'an.
- Huanza kwa kauli; mfano: Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema, Allah (s.w) amesema, "….." *Matin yake ni kauli ya Allah katika "……".*

- **Tanzu (makundi) za Hadith.**
  - **Tanzu za Hadith kutokana na Usahihi.**
    - Kutokana na usahihi, hadith zimegawanyika makundi manne;

1) Hadith Sahihi.

- Ni Hadith zenye wasimulizi wote wenye sifa zilizokamilika na kuwa na matini sahihi.

2) Hadith Hasan.

- Ni Hadith zenye matini sahihi lakini baadhi ya wasimulizi wake

wamekuwa dhaifu.

3) Hadith Dhaifu.

- Ni Hadith yenye matini sahihi lakini miongoni mwa wasimulizi wake wanakasoro kubwa zilizojitokeza.
- Hadith za namna hii haziaminiki na si za kutegemea.

4) Hadith Maudhu'u.

- Ni Hadith ya uwongo ambayo Mtume (s.a.w) amezuliwa nayo.
- Hizi ni Hadith zinazopingana na Qur'an na Hadith zilizo sahihi pia.

- **Tanzu kutokana na Umashuhuri (Umaarufu).**

- Kutokana na Umashuhuri, Hadith zimegawanyika makundi mawili;

1) Hadith Mutawatir.

- Ni Hadith yenye kusimuliwa na watu wengi kwa nyakati tofauti, wanne au zaidi wote wakiwa na sifa kamili.
- Hadith hizi ni ndio zenye kukubalika na watu wote.

2) Hadith Ahad.

- Ni Hadith ambayo ina wasimulizi wenye sifa zilizokamilika, lakini hawana mfungamano au msururu wa wasimulizi una mapengo kati kati.

- Ni Hadith zisizokubalika kwa watu wengi, ni za mashaka mashaka na si za kutegemea.

6.3 Mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa.

- Rejea Kitabu cha 2, EDK, Shule za Sekondari; Uk.226 - 232.

Zoezi la 6.

1. (a) Nini maana ya Hadith kilugha na kisheria.

(b) Eleza kwa muhtasari maana ya maneno yafuatayo:

(i) Matin (ii) Isnad (iii) Riwaya (iv) Hadith Qudussiyu. (v) Hadith Ahad.

2. (a) Wakati wa Mtume (s.a.w), hapakuwepo na uandishi wa Hadith. Toa sababu tano.

   (b) Ni sababu zipi zilizopelekea uandishi wa Hadith kuwa na hitajio kubwa katika kipindi cha Maswahaba?

3. (a) Taja vitabu viwili vilivyoandikwa pamoja na waandishi wake katika kipindi cha Maswahaba.

   (b) (i) Orodhesha maimamu wanne mashuhuri waliojitokeza kwa uandishi wa Hadith katika kipindi cha Tabi'ina.

   (ii) Taja majina ya Vitabu viwili na maimam walivyoviandika katika kipindi cha Tabi'ina.

4. Bainisha kwa muhtasari maimam sita waliojitokeza katika kipindi cha Tabi'i Tabi'ina.

5. Eleza kwa ufupi yafuatayo;

   (a) Al-Qatadaya (b) Al-Muwattah (c) Hadith Nnabawwi (d) Hadith Mutawattir.

6. (a) Maimam sita walioandika ***"Sahihu Sitta",*** vitabu vyao vinamadaraja tofauti ya usahihi wa Hadith. Changanua madaraja hao kutokana na usahihi wa Hadith.

   (b) Ni yapi masharti yaliyotumika katika kuhakiki usahihi wa Hadith?

   (c) Bainisha aina kuu za Hadith.

7.0 BARA ARAB ZAMA ZA JAHILIYYAH, KARNE YA 6 A.D.

7.1 Hali ya Bara Arab zama za Jahiliyyah.

- **Jiografia ya Bara Arab.**

- Bara Arabu imezungukwa na bahari katika tatu, Magharibi kuna bahari ya Shamu, Mashariki kuna Ghuba ya Uajemi na Oman, Kusini kuna bahari ya Uarabuni na Kaskazini ni Jangwa la Syria.

- Bara Arabu liko kati kati ya mabara matatu; Asia, Ulaya na Afrika.
- Saudi Arabia ndio nchi kubwa kuliko zote Bara Arabu ambamo kuna miji mitakatifu ya Makkah na Madinah.

- **Hali ya Maadili na ushirikina katika jamii wakati wa kuzaliwa Mtume (s.a.w).**

- Wakati anazaliwa Mtume mwaka 570 A.D (karne ya 6 A.D) dunia nzima ilikuwa katika giza totoro la ujahili.

- Maisha ya jamii yalikuwa yanaendeshwa kibabe na kibinafsi kwa kufuata matashi ya nafsi zao.

- Ubabe, ukandamizaji, unyonyaji, uporaji na dhuluma katika maisha yalionekana kama matendo ya kishujaa na kujivunia.

- Walizama katika ushirikina kiasi cha watu kuweza kutembea na miungu mifukoni mwao.
- Hali hii ya giza totoro ilienea pia nchi na mabara mbali mbali ulimwenguni kote.

- Dini kubwa zilizokuwepo muda huo zilikuwa ni Uyahudi na Ukristo lakini hazikuweza kumkomboa mwanaadamu kwa lolote hata kidogo.

- Hapakuwa na serikali, kila kabila lilikuwa na kiongozi na taratibu zake katika kuendeshea maisha.

- Unyanyasaji wa wanawake kila nyanja, mauwaji ya watoto wa kike wakiwa hai ilikuwa ni desturi ya kawaida katika maisha ya jamii ya Waarabu.

- **Mji wa Makkah na Kabila la Kiqureish.**

  - Mji wa Makkah ni mji mkongwe wa kihistoria ulioanzishwa na Nabii Ibrahiim miaka mingi iliyopita.

  - Nabii Ibrahim (a.s) na mwanae Nabii Ismail (a.s) ndio walioinua kuta za nyumba tukufu ya Ka'abah kwa amri ya Allah (s.w).
    Rejea Qur'an (2:127).

  - Ka'abah ni nyumba ya mwanzo na pekee ulimwenguni iliyowekwa kwa ya kuhiji wanaadamu wote ulimwenguni.
    Rejea Qur'an (22:27), (3:96) na (22:29).

  - Kutokana na jangwa na ukame wa mji huu, Allah (s.w) alijaalia chem.-chem ya maji ya zamzam kutokana dua ya Nabii Ibrahim (a.s).
    Rejea Qur'an (14:37).

  - Mji huu ulipata utukufu kutokana na uwepo wa nyumba tukufu ya Ka'aba ambapo kabila la Qureish ndio walikuwa walinzi wa nyumba hiyo.
    Rejea Qur'an (106:1-4).

  - Ni mji alikozaliwa Mtume Muhammad (s.a.w) mwaka 570 A.D katika kabila la Kiqureish mwaka wa ndovu.
    Rejea Qur'an (105:1-5).

  - Kabila la Kiqureish liliheshimika kuliko makabila mengine kwa huduma walizokuwa wakitoa kwa watu wanaohiji, misafara ya biashara na kule kuitumikia nyumba hiyo.

  - Kabila la Qureish ni miongoni mwa makabila ya waarabu yaliyojishughulisha sana na biashara mbali mbali ndani na nje ya Makkah kwa muda mrefu.

7.2 Kuandaliwa Mtume (s.a.w) Kulingania Uislamu katika mji wa Makkah.

- **Nasaba ya Mtume (s.a.w).**

  - Mtume (s.a.w) alizaliwa siku ya kuamkia Jumatatu, tarehe 20 mwezi April, 570 A.D. sawa na mwezi 12 Rabi'ul-Awwal, mwaka wa tembo.

  - Muhammad (s.a.w) alizaliwa katika kabila la Quraish, baba yake ni Abdullah bin Abdul-Muttalib, aliyefariki kabla ya kuzaliwa kwake.

  - Mama yake Muhammad (s.a.w) ni Amina bint Wahhab, ambaye ni miongoni mwa koo za Kiqureish pia.

  - Uzaliwa wa Muhammad (s.a.w) una nasaba na kizazi cha Nabii Ismail (a.s), alipozaliwa alipewa jina la 'Muhammad' au 'Ahmad' lenye maana ya mwenye kusifiwa kwa vitendo vizuri.

- **Malezi ya Mtume (s.a.w).**

  - Muhammad (s.a.w) baada ya kuzaliwa, alinyonyeshwa na kulelewa na Bibi Halimah bint Dhayb kutoka mji wa Taif, kutokana na hali ya hewa safi ya huko mpaka alipofikia umri wa miaka miwili.

  - Muhammad (s.a.w) alirejeshwa Makka na alikaa na mama yake muda wa miaka 6 naye alifariki 576 A.D. hapo akawa chini ya malezi ya babu yake Abdul-Muttalib aliyefariki mwaka 578 A.D. Muhammad (s.a.w) akiwa na miaka 8.

  - Baada ya kufariki babu yake, Muhammad (s.a.w) akawa chini ya malezi ya ami (baba mdogo) yake Abu Talib mpaka alipopata Utume.

- **Kuandaliwa Muhammad (s.a.w) kabla ya kupewa Utume.**

  - Maandalizi (mafunzo) haya yalikuwa ya **Kiil-hamu** ambayo hata Muhammad mwenyewe na jamii haikujua kuwa anaandaliwa, na yalikuwa kama ifuatavyo;

    i. Kuzaliwa katika kabila tukufu la Kiqureish ambalo ni kizazi cha Nabii Ibrahim (a.s) kupitia kwa Nabii Ismail (a.s).
    Rejea Qur'an (2:129).

    ii. Kupewa jina la Muhammad na babu yake lililo na maana sawa na 'Ahmad'- Mshukuriwa, alilotabiriwa nalo katika Injili, na Qur'an pia.
    Rejea Qur'an (61:6).

    iii. Malezi bora aliyopata kupitia Mama yake mzazi, Bi Halimah, babu yake Abdul-Muttalibu na Ami ya Abu Talibu pamoja na kuwa alikuwa yatima.
    Rejea Qur'an (93:6).

    iv. Tabia yake njema isiyo na mfano kuanzia utotoni hadi utuuzima wake kutoathiriwa na kila aina ya ubaya.
    Rejea Qur'an (68:4).

    v. Ndoa yake Muhammad (s.a.w) na Bi Khadija bint Khuwailid, aliiandaa Allah (s.w) ili kumuwezesha Muhammad kuitumikia jamii hata kabla ya utume.
    Rejea Qur'an (93:8).

    vi. Kuchukia kwake maovu na kujitenga pangoni ili kutafuta msaada ulio nje ya uwezo wa kinaadamu baada ya kufanya jitihada mwisho wa uwezo wake.
    Rejea Qur'an (93:7) na (94:1-3).

Mafunzo yatokanayo na maandalizi haya ya Ki-Ilhamu

i. Hatuna budi kuwaandaa watoto wetu kuwa Makhalifah (viongozi) wa Allah (s.w) hata kabla hawajazaliwa.

ii. Hatuna budi kuwaandaa walimu (madai'yah) watakaoufundisha Uislamu na taaluma zingine kwa lengo la kuusimamisha Uislamu katika jamii.

iii. Hatuna budi kushirikisha familia zetu kwenye harakati za kuuhuisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii.

iv. Wanawake wa Kiislamu hawanabudi kumuiga Bi Khadija, mkewe Mtume (s.a.w) katika kuwasaidia waume zao katika harakati za kuupigania Uislamu.

v. Pia hatuna budi kuchukia kila aina ya uovu na dhuluma unaofanywa katika jamii, na tujitahidi kuyaondoa kwa mikono na kauli zetu kabla ya kujitenga.

vi. Hatuna budi pia kujipamba na kila tabia na mwenendo mwema kwa kadri ya uwezo wetu.

vii. Pia hatuna budi kujiimarisha kiuchumi kwani ndio ni katika nyenzo kuu za kuweza kuusimamisha na kuuendeleza Uislamu katika jamii.

- **Kuandaliwa Muhammad (s.a.w) wakati na baada ya kupewa Utume.**

  - Maandalizi haya yalikuwa ya kimafunzo (maelekezo) yaliyotokana na wahay moja kwa moja ulipokuwa unamshukia, ulianza katika sura tatu zifuatazo;

    - **Suratul-A'laq (96:1-5).**
      - Huu ulikuwa wahay wa kwanza kabisa kumshukia Muhammad (s.a.w)

kama ifuatavyo;

"Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba, Amemuumba mwanaadamu kwa Alaq (pande la damu). Soma, na Mola wako ni Karimu sana. Ambaye amemfundisha (elimu zote) kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui."

- **Suratul-Muzzammil (73:1-10).**
  - Huu ulikuwa wahay wa pili kumshukia Mtume (s.a.w) kama ifuatavyo;

"Ewe uliyejifunika maguo! Simama usiku (kucha kufanya ibada), ila muda mdogo (tu hivi) nusu yake au ipunguze kidogo au izidishe na soma Qur'an vilivyo. Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito. Hakika kuamka usiku (na kufanya ibada) kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno (yake) yanatua zaidi. Hakika mchana una shughuli nyingi. Na litaje jina la Mola wako na ujitupe kwake kwa kweli. (Yeye ndiye) Mola wa mashariki na magharibi, hakuna muabudiwa wa haki ila Yeye, basi mfanye kuwa mlinzi (wako). Na subiri juu ya hayo wasemayo (hao makafiri) na uwaepuke mwepuko mwema."

- **Suratul-Muddaththir (74:1-7).**
  - Huu ulikuwa ni wahay wa tatu kumshukia Mtume (s.a.w) kama ifuatavyo;

"Ewe uliojifunika maguo. Simama na uonye (watu) na Mola wako umtukuze. Na nguo zako uzisafishe (uzitwaharishe). Na mabaya yapuuze. Wala usiwafanyie watu ihsani (viumbe) ili upate kujikithirisha. Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira."

Mafunzo yatokanayo na Maandalizi ya Mtume (s.a.w) Kimafunzo (Ki-wahay).

i. Elimu katika fani zote (isipokuwa uchawi) ndio nyenzo kuu katika maandalizi kuusimasha Uislamu katika jamii.

ii. Kisimamo cha usiku kufanya ibada, ni katika nyenzo kuu ya pili katika maandalizi ya kusimamisha Uislamu katika jamii.

iii. Kusoma Qur'an kwa mazingatio kwa lengo la kuifanya muongozo pekee wa maisha pia ni maandalizi ya kuutawalisha Uislamu katika jamii.

iv. Kumtaja na kumtukuza Allah (s.w) vilivyo, pia ni katika nyenzo na maandalizi katika kuusimamisha Uislamu ndani ya jamii.

v. Kujitupa kwa Allah (s.w) kwa kweli – ni kumcha Allah (s.w) peke yake ukweli wa kumcha, nayo ni katika maandalizi ya kusimamisha Uislamu. Rejea Qur'an (3:102).

vi. Kumfanya Allah (s.w) ndiye mlinzi pekee na kumtegemea, ni jambo la muhimu katika kusimamisha Uislamu katika jamii.

vii. Kusimama na kuonya (kulingania Uislamu), ni jambo muhimu sana linalowezesha Uislamu kufahamika kwa watu.

viii. Kutakasa (kutwaharisha) nguo ni amri ya Allah (s.w) inayomtaka kila mlinganiaji wa Uislamu kuwa safi wa kuigwa kimwili na kiroho pia. Rejea Qur'an (41:33).

ix. Kupuuza na kujitenga na mabaya na wabaya ni jambo la muhimu ili kukataza kwake maovu kuwe na athari.

x. Kufanya ihsani (wema) kwa ajili tu kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w) ndio uhai wa ibada ya muislamu.

xi. Kufanya subira kwa ajili ya Allah (s.w) ni katika nyenzo kuu katika kupelekea kuusimamisha Uislamu katika jamii.

xii. Utekelezaji wa ujumbe wa Qur'an ni kazi nzito na yenye kila aina ya misukosuko, hivyo kuwa na subira ndio nyenzo pekee.

7.3 Mtume (s.a.w) Kuulingania Uislamu Makkah kwa siri.

- Mtume (s.a.w) alianza kulingania familia yake, kisha rafiki zake na jamaa zake wa karibu walio rafiki.

- Mtume (s.a.w) alianza kulingania Uislamu kwa siri kwa muda wa miaka mitatu kwa kukutana na waislamu waliosilimu mwanzo kabisa katika nyumba ya bwana **Arqam bin Arqam** – maarufu kama **Darul-Arqam**.

- **Mtume (s.a.w) kuutangaza Uislamu Makkah kwa jamii nzima.**

  - Baada ya miaka mitatu ya kuulingania Uislamu kwa siri, aliamrishwa kuutangaza sasa hadharani kwa jamii yote inayomzunguka.

  - Mara tu baada ya Mtume (s.a.w) kuutangaza ujumbe wa Uislamu hadharani, alikumbana na Upinzani dhidi ya ujumbe wake huo kutoka kwa Makafiri wa Kiqureish wa Makkah.

    - **Sababu za Makafiri wa Kiqureish kuupinga ujumbe wa Uislamu.**

      i. Walihofia kupinduliwa mfumo wao wa utawala kandamizi na kusimama mfumo wa Uislamu unao simamia haki na uadilifu.

ii. Walihofia kupoteza maslahi yao kupitia njia kandamizi, nyonyaji na haramu katika jamii zao.

iii. Walihofia kukosa wafuasi ambao ndio ilikuwa rasilimali pekee katika kuendeleza na kuimarisha unyonyaji wao.

iv. Walihofia kupoteza nafasi yao katika kuiongoza jamii kama fursa pekee ya kunyonya, kudhulumu na kulinda maslahi yao.

v. Walihofia kupoteza umaarufu na nafasi ya ibada (itikadi) zao za kishirikina ambazo ndizo nyenzo pekee za mapato yao.

- **Mbinu walizotumia Makafiri wa Kiqureish katika kuupinga Uislamu Makkah.**

- Maqureish wa Makkah walitumia kila mbinu kuhakikisha kuwa ujumbe wa Uislamu haufiki na kukubalika katika jamii yao, miongoni ni hizi zifuatazo;

a) Kumkatisha tamaa Mtume (s.a.w) na wafuasi wake.

- Makafiri walimdhihaki Mtume (s.a.w) na waumini wachache kwa kumuita majina mabaya kama; mwendawazimu, mtunga mashiri, aliyepagawa na mashetani, mchawi, n.k.

- Pamoja na kusimangwa huko Mtume (s.a.w) na waislamu hawakukata tamaa, waliendelea kuutangaza Uislamu katika jamii yote.

b) Mbinu ya Vitisho na Kumkataza Mtume (s.a.w) kuulingania Uislamu kwa kumtumia Ami yake, Abu Talib.

- Wakuu wa Maquraish walimuagiza Abu Talib amkataze Muhammad (mwanae) kuendelea kuutangaza Uislamu kwa kumbadilishia mtoto mwingine la sivyo watamshambulia yeye na Muhammad (s.a.w).

- Mbinu hii haikufanikiwa badala yake Abu Talib alimuunga mkono Mtume (s.a.w) kwa kazi yake baada ya kujua msimamo wake.

c) Mbinu ya Kumhonga na kumrubuni Mtume (s.a.w).

- Maquraish walitumia diplomasia kwa kumtaka Mtume (s.a.w) aache kazi ya kuutangaza Uislamu kwa kumpa kati ya vitu vifuatavyo; utajiri, mwanamke mzuri, madaraka au yote kama akitaka.

- Mtume (s.a.w) aliwakatalia vyote hivyo kwa kumsomea aya za Qur'an (41:1-37) mjumbe aliyetumwa kazi hiyo, Utbah bin Rabi'ah.

d) Mbinu ya kutaka kumlaghai Mtume (s.a.w).

- Maqureish walimletea Mtume (s.a.w) pendekezo kuwa washirikiane katika ibada kwa awamu, mwaka mmoja wamuabudu Mungu mmoja kwa pamoja na mwaka unaofuatia waabudu miungu yao pamoja pia.

- Hapo ndipo iliposhuka suratul-Kafiruun kuvunja pendekezo lao hilo la kushiki katika ibada na Mtume akawasomea aya za Qur'an kukataa. Rejea Qur'an (109:1-6) na (10:15).

e) Mbinu ya Kuwatesa na kuwaua Waislamu.

- Baada ya Maqureish kuona mbinu zote zimefeli, walianza kutumia nguvu na mabavu kuwatesa, kuwanyonga na kuwaua Waislamu waliong'ang'ani imani yao kama akina; Bilal bin Rabbah, Sumaiyya, Ammar bin Yasir na baba yake, n.k.

- Pamoja na mateso na mauaji, waislamu walibakia na msimamo wao bila kutetereka na kukata tamaa.

f) Mbinu ya fitina, kuipinga Qur'an na kuzuia watu kukutana na Mtume (s.a.w).

- Maquraish kwa kuhofia ujumbe wa Qur'an kuenea kwa watu, walianza kuzuia watu kwenda kuonana na Mtume (s.a.w) kwa kuwashawishi kuwa wasisikilize aya za Qur'an kwani ni uchawi, mashairi ya Muhammad.

- Walizidi kufitinisha kwa kumzuia Mtume (s.a.w) kuswali na kuwaambia watu kuwa Muhammad anapinga ibada na miungu wenu, lakini mbinu na ushawishi wao ulifeli pia.
  Rejea Qur'an (31:6), (41:26), (10:38), (11:13) na (96:9-19).

g) Mbinu ya kuwatenga na kila huduma ya kijamii.

- Maquraish walizidi kuongeza mateso kwa waislamu kwa kutenga na kuwafukuza Makka na kwenda kuishi katika jangwa la Shi'ab miaka mitatu bila chakula wala mahusiano mengine ya kijamii.

- Mbinu pia ilifeli baada ya baadhi ya Maquiesh kuona huruma kwa ndugu zao waliotengwa bila sababu za msingi, hivyo wakavunja mkataba wa kuwatenga.

h) Mbinu ya kutaka kumuua Mtume (s.a.w).

- Maquish waliazimia kumuua Mtume (s.a.w) na rafiki yake Abubakar (r.a) walipogundua kuwa waislamu wamehamia mji wa Madinah.

- Mbinu hii pia ilifeli baada ya Allah (s.w) kuwanusu katika pango yeye na sahibu yake Abubakar (r.a).
  Rejea Qur'an (9:40).

Mafunzo yatokanayo na Upinzani wa Maquraish dhidi ya Uislamu (Qur'an).

i. Upinzani wa Makafiri dhidi ya ujumbe wa Uislamu upo nyakati na muda wote na hautaisha.

ii. Hatuna budi kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa kuanzia familia, ndugu na jamaa zetu wa karibu kabla ya wengine ili kupata wasaidizi wa karibu.

iii. Waislamu hawana budi kuwa tayari na kutokata tamaa katika kuusimamisha Uislamu bila ya kumchelea yeyote yule.

iv. Makafiri siku zote wako tayari kutumia kila mbinu na njia kuhakikisha kuwa wanabaki katika utawala na itikadi za ibada zao ili kuendeleza na kuimarisha maslahi yao kupitia unyonyaji na ukandamizaji.

v. Mbinu za Makafiri za kutaka kuuhilikisha Uislamu na waislamu zinafanana katika zama zote za historia ya maisha ya mwanaadamu.

vi. Mtume (s.a.w) na maswahaba wake waliweza kuhimili vitimbi vya makafiri na hatimaye kuweza kuusimamisha Uislamu katika jamii ni baada ya wao kufuata na kutekeleza kikamilifu mafunzo ya Qur'an (96:1-5), (73:1-10) na (74:1-7).

vii. Suala la kuulingania na kuutangaza ujumbe wa Uislamu ni zito, lenye misukosuko na gharama kubwa ya kutoa mali na nafsi (uhai).

viii. Siku zote makafiri na maadui wengine wa Uislamu hawakotayari kuona Uislamu unasimama katika jamii na waislamu wanautekeleza vilivyo.

ix. Tusitarajie matunda ya kusimama Uislamu kupatikana kwa muda mfupi na kwa urahisi, kwani linahitaji mipango ya muda mrefu na kujitoa muhanga.

x. Wakati wowote Waislamu watakapojizatiti katika kuulingania na kuupigania Uislamu kwa mali na nafsi zao, Allah (s.w) atawapa nusura dhidi ya maadui wao.
Rejea Qur'an (61:8, 10-13).

- **Mtume (s.a.w) alivyoandaa Ummah wa Kiislamu Makkah.**

- Mtume (s.a.w) alitumia kila aina ya fursa iliyopatikana katika kuufikisha ujumbe Uislamu kwa watu wengine.

- Mtume (s.a.w) alifikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu na makabila mbali mbali kwa siri na dhahiri kutokana na uadui wa Maquraish dhidi yake.

- Mtume (s.a.w) alitumia mikataba kwa kuandaa ummah wa kiislamu kutoka sehemu mbali mbali hasa mji wa Madinah (Yathrib) kama ifuatavyo;

  - **Mikataba ya 'Aqabah.**

    - Hii ilikuwa ni baina ya Mtume (s.a.w) na watu wanaotoka nje ya mji wa Makkah hasa waliokuja kuhiji msimu wa Hija.

    - Mtume (s.a.w) alikutana na kikosi cha kwanza kabisa cha watu sita (6) kutoka Madinah (Yathrib) wa kabila la Khazraj, baada ya kuwafikishia ujumbe wa Uislamu, walisilimu na wakaahidi kuufikisha kwao Madina.

    - Mwaka uliofuata, **621 A.D**, kikundi kingine cha waislamu 12 (2 Aus na 10 Khazraj) walikutana na Mtume (s.a.w) kwa siri eneo la **'Jaratul 'Aqabah'** na kuweka **mkataba wa kwanza wa 'Aqaba** na kukubaliana yafuatatayo;

      i. Hawataabudu chochote isipokuwa Allah (s.w) pekee.
      ii. Hawataiba wala hawatapokonya misafara ya biashara njiani.
      iii. Hawatazini.

iv. Hawatawaua watoto wao tena.

v. Hawatasema uongo wala hawatawasingizia wengine uovu.

vi. Hawatamuasi Mtume kwa kila atakalowaamrisha na watakuwa waaminifu kwake kwa hali yeyote iwayo.

- Mtume (s.a.w) aliwapa mwalimu wa kuwafundisha Uislamu, 'Mus'ab bin Umair.

- Mwaka uliofuata, **622 A.D**.walimjia Mtume (s.a.w) waislamu 75 (wanawake 2) wakiongozwa na mwalimu wao, 'Mus'ab na kufunga **Mkataba wa pili wa 'Aqabah** sehemu ile ile kwa kukubaliana kuwa;

  - *Mtume na Waislamu wote wa Makka wahamie Madinah (Yathrib) na wao watawapokea na kuwahifadhi dhidi ya maadui wao.*

- Mtume (s.a.w) aliwachagulia viongozi 12 (9 Khazraj na 3 Aus) na watu watakaokuwa chini ya kila kiongozi, na wanaume wote walimpa Mtume (s.a.w) mkono wa bai'at kwa maana ya utii wao kwake.

- Baada ya kikundi hicho kurejea na kufika Madinah salama, ndipo Mtume (s.a.w) aliwatangazia waislamu wote wa Makkah kuhamia Madinah.

- Na takriban baada ya miezi miwili hivi, Waislamu wote wenye uwezo wa kuhama walishahamia Yathrib (Madinah) kwenda kujiimarisha zaidi.

Mafunzo yatokanayo na Mikataba ya 'Aqabah katika kuandaa ummah.

i. Waislamu hawana budi kupanga mikakati na mambo yao kwa siri ili kutojulikana na maadui wa Uislamu na waislamu.

ii. Waislamu hawanabudi kutotangaza mikakati yao kwa maadui kabla ya kuitekeleza ili kuepukana na njama ya kukwamishwa.

iii. Waislamu hawanabudi kuwa na mipango na mikakati (long and short term strategies) ya muda mrefu na mfupi katika kuandaa Ummah.

iv. Uongozi bora na makini ni jambo la msingi sana la mwanzo katika kuusimamisha na kuuendeleza Uislamu katika jamii.

v. Waislamu wanaharakati wanapoazimia jambo lolote katika kuusimamisha na kuuendeleza Uislamu, hawana budi kujifunga nalo na kupeana kiapo cha utekelezaji.

vi. Waislamu hawana budi kutumia kila aina ya fursa itakayojitokeza katika kuusimamisha na kuuendeleza Uislamu katika jamii.

- **Maandalizi ya Hijra ya Mtume (s.a.w) na Waislamu kuhamia Madinah.**
  - Mtume (s.a.w) hakuhama mpaka alipoletewa amri ya kuhama, na aliindaa safari yake kistretejia akiwa sahibu wake Abubakar (r.a).

  - **Mikakati na Maandalizi ya Kistretejia** aliyofanya Mtume (s.a.w) na Abubakar (r.a) kabla ya kuanza safari ya kuhama kwenda Yathrib (Madina);

    i. Walipanga kuwa watajificha katika pango Thaur kwa siku tatu kabla ya kuanza safari ya kuelekea Yathrib (Madinah).

    ii. Walipanga kutumia njia ya uficho isijulikana na mtu ya kuelekea kusini badala ya njia ya kawaida ya kuelekea kaskazini.

    iii. Walimkodi bedui mweledi wa njia ile atakayewaongoza mpaka Yathrib kwa dinari 300.

iv. Abubakar (r.a) alinunua ngamia wawili kwa ajili ya safari yake na Mtume (s.a.w).

v. Abubakar (r.a) alimchukua bint yake Asma kwa siri ili kumuonyesha pango lilipo na awe anawaletea chakula muda watakapo kuwa pangoni.

vi. Pia Abubakar (r.a) alimwagiza mchunga mbuzi wake awe anachungia karibu na pango ili awapatie maziwa.

vii. Abubakar (r.a) pia alimpa jukumu kijana wake Abdullah kuwaletea taarifa za mjini kwa yatakayojitokeza baada ya wao kuondoka.

- Maquraish baada ya kubaini kuwa waislamu wameshahamia Yathrib, na Mtume (s.a.w) anajiandaa naye ahame, walipanga njama ya kumuua kabla hajahama.

- Maquraish walichagua vijana shupavu kutoka kila ukoo wa kiquraish na kuwapa mapanga makali ili wajewamvamie kwake akiwa amelala usiku kwa pamoja ili lawama ya kumuua isiangukie ukoo mmoja.

- Kabla ya kuondoka, Mtume (s.a.w) alimkabidhi Ali (r.a) amana zote za watu ili kuwarejeshea na akamwamuru alale katika kitanda chake.

- Allah (s.w) alimnusu na kabla ya Alfajir, Mtume (s.a.w) aliondoka pamoja na Abubakar (r.a) kuelekea pangoni akawaacha ‘wauaji’ nje ya nyumba yake wamelala fofofo.

- Kufeli kwa zoezi la kumuua Mtume (s.a.w), Maquraish walitangaza zawadi ya ngamia 100 kwa atakaye mleta Muhammad au Abubakar yuko hai au amekufa.

- Maquraish kwa kumkodi bedui mjuzi wa kufuatilia nyayo, akiwaongoza mpaka pangoni lakini Allah (s.w) aliwanusu. Rejea Qur’an (9:40).

- Mwishowe baada ya siku tatu, Mtume (s.a.w) na sahibu wake, Abubakar (r.a) waliondoka kuelekea Madinah na walifika salama kabisa.

- Kwa heshima ya Mtume (s.a.w), mji wa Madinah ukawa unaitwa 'Madinatul-Munwwarah' (mji ung'aao).

- Baada ya kufariki (kutawafu) Mtume (s.a.w), Waislamu walikubaliana kuanzisha Kalenda ya mwaka wa Kiislamu **'Al-Hijrah' (A.H)** ianzie siku ile aliyohama (hijra ya) Mtume (s.a.w) kwenda Madinah.

Mafunzo yatokanayo na Hijrah ya Mtume (s.a.w) na Maswahaba wake.

i. Hatuna budi kutunza na kurejesha amana za watu kwa wenyewe bila kujali uadui wao kwetu.

ii. Waislamu hawanabudi kuweka mipango na mikakati madhubuti juu ya namna ya kutekeleza mambo yao kabla ya utekelezaji wake.

iii. Waislamu hawana budi kuchukua tahadhari katika kuendesha harakati za kidini kwa kuzingatia kuwa dini ya Uislamu ina maadui wengi.

iv. Nusura ya Allah (s.w) na Ushindi hupatikana tu baada ya kufanyika jitihada za dhati katika kuusimamisha Uislamu katika jamii na kumtegemea yeye pia.

v. Waislamu wanalazimika kufanya jitihada ya dhati ya kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo kwa kila kipengele cha maisha yao, kama mazingira yatakuwa ndio kikwazo hawanabudi kuhama (kuhajiri) kwenda sehemu (ardhi) yenye wasaa. Rejea Qur'an (4:97-99).

vi. Kuhajiri (kuhama) kwa ajili ya Uislamu sio ukimbizi, bali ni katika mikakati na mipango ya kwenda kujiimarisha huko na hatimaye kuja kukomboa sehemu mlikotoka.

vii. Kutokana na Hijrah ya Mtume (s.a.w), tunajifunza kuwa waislamu wote ni ndugu mmoja bila ya kujali kabila, rangi, taifa, n.k.

viii. Uislamu siku zote hauwezi kusimama katika jamii mpaka waislamu tuwe tayari kujitoa muhanga kwa mali na nafsi zetu kadri ya uwezo wetu.

ix. Ni haramu kwa muislamu kuishi katika nchi ya kikafiri au utawala wa kikafiri isipokuwa, itakapokuwepo jitihada ya kuundoa ukafiri na kuutawalisha Uislamu au yatakapokuwepo maandalizi ya kuhama sehemu hiyo.

Zoezi la 7.

1. (a) Nini maana ya 'zama za Jahiliyyah'?
   (b) Bainisha baadhi ya mambo aliyoyakuta Mtume (s.a.w) katika jamii ya waarabu wa Makkah zama za Jahiliyyah.
2. Mji wa Makkah ni mji mkongwe na mtukufu tangu zama za Nabii Ibrahim (a.s). Thibitisha kauli hii kwa kutoa sababu ya utukufu wa mji wa Makkah.
3. (a) Bainisha sababu zilizopelekea Muhammad (s.a.w) alipokuwa mdogo kwenda kulelewa nje ya mji wa Makkah.
   (b) Taja baadhi ya sifa au tabia za Mtume (s.a.w) alizokuwa nazo tangu utotoni zilizokuwa kama ishara ya kuandaliwa kuwa Mtume wa Allah.
4. (a) Bainisha maandalizi ya Mtume (s.a.w) kabla ya kupewa Utume (mafunzo ya Ki-Ilhamu).
   (b) Ni yapi mafunzo yatokanayo na Maandalizi ya Mtume (s.a.w) ya Ki-Ilhamu?
5. Mtume (s.a.w) alianza kupewa mafunzo ya Ki-wahyi mara tu baada ya kuanza kumshukia sura tatu za mwanzo, (96:1-5), (73:1-10) na (74:1-7).

Kutokana na aya hizi ainisha mafunzo yatokanayo.

6. (a) Ni sababu zipi za msingi ziliwafanya Maquraish wa Makkah kuupinga Ujumbe wa Qur'an?
   (b) Ainisha njia na mbinu walizotumia Maquraish katika kuupinga na kuuzuia ujumbe wa Uislamu kuenea katika jamii na mafunzo yatokanayo.

7. Changanua njia alizotumia Mtume (s.a.w) katika kuandaa ummah wa Kiislamu Makkah kwa kutumia mikataba ya 'Aqabah.

8. Katika kuendesha harakati za kuusimamisha Uislamu, hatuna budi kuwa na mikakati madhubuti. Kwa kurejea historia ya Mtume (s.a.w) onyesha jinsi alivyotumia stretejia madhubuti wakati wa kuhama kwenda Madinah.

9. 'Hijra katika Uislamu si sawa na Ukimbizi, bali na stretejia za kuunganisha nguvu ya kuusimamisha Uislamu'.
   Kwa kutumia Hijra ya Mtume (s.a.w), mambo gani waislamu wa leo tunajifunza katika hatua za kuupigania Uislamu.

****

Wabillah Tawfiiq

****